SUPA JACKPOT
TZS. 1,154,861,566
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Samia:** Ruzuku tunayowapa ni ya miaka michache tu

UKURASA 2


Ukurasa 12
Tanzania ya kidijitali program itakayoleta zama kiteknolojia
Ukurasa 13
Taulo za kike zilivyojibu kwa kupandisha taaluma
Nipashe TESA
Jumanne Septemba 19, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Ukurasa 14
Alois Alzheimer; mtaalamu nguli mgunduzi wa maradhi ya usahaulifu
ELIMU
NA SALUMU MATATA, UDSM
TAIFA KINARA ULEVI
Ije tena 'operesheni tokomeza viroba' kukabili 'pepo' kulewa kupindukia
AFYA ni tunu isiyoweza kulinganishwa na chochote, tena inayostahili kulindwa kwa juhudi zote kwani ndiyo uzima na chachu ya kumudu maisha kwa kufanyakazi hasa kwa kundi la nguvu kazi vijana na watu wazima.
Kwa taifa lolote nguvu kazi tegemeo ni vijana wanaoleta maendeleo ya nchi kwa kufanyakazi kuanzia mashambani, mijini na vijijini. Nchi isiyo na vijana ni kama imepungukiwa rasilimali muhimu.
Wiki inapoanza bado wengi walioumaliza juma na taarifa za vijana kunywa pombe kupindukia bado wanatafakari kwa kina.

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Septemba 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581438
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# CHADEMA yapinga tozo kwenye petroli

• **Yataka** mikataba ya gesi asilia iwekwe wazi; EWURA wakunjua makucha... *Endelea ukurasa 3&4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**ZIARA YA RAIS; WIZARA YATUMBUA VIGOGO SABA WA HALMASHAURI**

UKURASA WA 19
MAUAJI YA DADA BILIONEA MSUYA
**WAKILI ADAI DADA WA KAZI ALISAIDIA TUKIO LA MAUAJI**



## Neema iliyojificha maboresho bima ya Toto Afya Kadi

UKURASA 5





# Amkata mwenza koromeo kisha ajiua kwa kisu tumboni

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI AIONYA YANGA, ATAKA MABAO UK.24 **KATUNI** UK.6

# Amkata mwenza koromeo kisha kujiua kwa kisu tumboni

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

MWANAMUME anayejishughulisha na ufundi ujenzi aliyefahamika kwa jina moja la Amos, anadaiwa kumuua mpenzi wake, Samira Mathias, kwa kumkata koromeo kisha kujichoma kisu tumboni kwa kile kilichodaiwa wivu wa mapenzi.

Tukio hilo lililothibitishwa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, linahusisha wapenzi hao walikuwa wanaishi Mtaa wa Oysterbay, Kata ya Makulu jijini Dodoma.

Inadaiwa kuwa mwanamke ndiye alikuwa amepanga katika chumba hicho na mwanamume alikuwa anakwenda na kuondoka.

Akizungumza na waandishi wa habari hizi, mashuhuda wa tukio hilo, akiwamo mwenye nyumba hiyo, Donald Nembele, walidai walisikia kelele ndipo walikusanyika na kuvunja mlango na kuona damu imetapakaa ndani huku mwanamke chini.

Nembele alisema kuwa walipoingia walikuta mwanamke akiwa na jeraha kubwa shingoni na mwanamume tumboni huku utumbo ukiwa nje.

Alisema baada ya kuona hali hiyo, alikwenda kutoa taarifa kwa kiongozi wa mtaa ambaye alishirikiana na majirani kutoa taarifa Kituo cha Polisi Chimwaga.

Balozi wa eneo hilo, Isaya Mabiliji, alidai ni tukio la kwanza la mauaji ya aina hiyo katika mtaa wake. Limeshtua wengi.

Alisema alikwenda eneo la tukio baada ya kuitwa na mwenye nyumba na alipofika, watu hao walionekana wameshafariki dunia. Hata hivyo, hana mamlaka kuthibitisha kifo.

"Kwa kweli inasikitisha sana kuona mauaji kama haya yanatokea mtaani kwetu, tena kwa vijana wadogo. Wawili hawa wanasadikiwa ni wapenzi na wamekuwa wakiishi kama mke na mume, hatujui walipatwa na nini," alisema.

Alisema taarifa za awali kutoka kwa majirani zinaeleza kuwa wapenzi hao waligombana kwa muda mrefu hadi baadaye zilitawala kelele na watu walivyovunja mlango walikutana na damu na miili ya wapenzi ikiwa na majeraha.

"Tukio kama hili sio zuri kabisa machoni mwa watu, ni muhimu watu wakaacha kuchukua sheria mkononi, ni hatari sana kufanya hivi kwa kuwa inaleta maumivu na kusababisha vifo," alisema Mabiliji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alisema uchunguzi wa awali unaonesha chanzo ni wivu wa mapenzi baina ya wapenzi hao.

"Kweli tukio hilo limetokea majira ya saa nane kwenda saa tisa usiku katika eneo hilo la Oysterbay ambako mwanamume aliyefahamika kwa jina moja la Amos amemuua mpenzi wake Samira Mathias kwa kumchoma kisu shingoni hadi kukata koromeo lake.

"Lakini baadaye mwanamume huyo naye alijichoma kisu tumboni hadi utumbo kutoka nje, na majirani walipovunja mlango walikuta analalamika walipokwenda kutoa taarifa polisi waliporudi walikuta mwanamume ameshafariki dunia," alisema Kamanda Otieno.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi wa tukio ambalo limesababishwa vifo vya wawili hao. Miili imehifadhiwa hospitalini.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Amina Khamis Shaaban, akipewa maelezo na Mkuu wa Kituo cha Utafiti na Majaribio wa Kampuni ya Hyundai Rotam, Dongjin Son, kuhusu hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mabehewa wakati ujumbe wa Tanzania ulipotembelea kiwanda hicho Changwon, Korea Kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia awakumbusha wakulima ruzuku ya mbolea itafika kikomo

**Na Jenifer Gilla**

Rais Samia Suluhu Hassan amesema ruzuku ya mbolea inayotolewa sasa hivi na serikali itafika kikomo miaka michache ijayo na kuwataka wananchi kununua kwa bei halisi ya soko.

Pia amewataka kuweka akiba ya fedha wanazopata kutoka kwenye mauzo ya mazao ili zisaidie kuendeleza shughuli za kilimo wakati ambao hakuna ruzuku.

Rais aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akiendelea na ziara yake mkoani Lindi.

Katika ziara hiyo aliweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara ya Ruangwa hadi Nanganga yenye urefu wa kilometa 53 na Jengo la Halmashauri ya Mtama.

"Ni muhimu kuwa na matumizi mazuri ya fedha zinazotokana na kilimo ili muinuke kiuchumi na muwe na uwezo wa kujitegemea kununua mbolea kwa kuwa misaada inayotolewa na serikali ina mwisho," alisema.

Akiwa katika viwanja vya Kilimahewa, wilayani Ruangwa, Rais Samia alisema serikali inafanya kazi kubwa kuwatengenezea mazingira mazuri katika kilimo, ikiwamo kuwapa mbolea ya ruzuku na kuwatafutia masoko kwa ajili ya kuwainua kiuchumi ila juhudi hizo zitagonga mwamba kama hawatokuwa na matumizi mazuri ya fedha.

Alisema serikali ipo katika mikakati ya kuboresha kilimo ikiwamo kupandisha thamani ya korosho, mbaazi na ufuta ili wakulima waweze kuuza bei nzuri na kuwasisitiza wakulima hao kuongeza uzalishaji.

Aliwataka kutumia umeme unaowekwa katika maeneo yao katika biashara ili kuboresha maisha yao badala ya kuutumia kwenye mambo yasiyo na tija.

Alisisitiza umuhimu wa kudumisha amani na utulivu ili kuwezesha viongozi kufanyia kazi miradi ya maendeleo, kwa kuwa kunapokuwa na uhasama na mapigano serikali itakosa muda wa kufanya mambo hayo badala yake itashughulikia migogoro yao.

**UMEME**

Alisema serikali inafanya kila jitihada rasilimali zilizopo mkoani humo ziwaletee maendeleo wananchi na kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji ili kuuletea mkoa wao maendeleo.

Alisema pia itaendelea kutoa fedha za maendeleo mkoani humo, ikiwamo Wilaya ya Ruangwa ambayo mwaka huu pekee imetoa Sh. bilioni 77 na zitaendelea kutolewa kwa kuwa serikali ipo kuwahudumia.

Alihakikisha kuwa serikali itafanya utafiti katika madini yanayopatikana mkoani humo ili kujua kiasi kilichopo na kuwajengea uelewa wachimbaji wadogo kuchimba kitaalam na kwa ajili ya maendeleo endelevu ya taifa.

Nanganga imeahidiwa kumaliziwa tatizo la umeme katika maeneo yaliyosalia nchini na kuwataka wautumie kujiletea manufaa na kujikwamua kiuchumi.

Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Kassim Majaliwa, alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kutoa fedha za kuendeleza miradi ya maendeleo katika mkoa huo ikiwamo ya elimu, afya, maji na barabara.

Alisema ingawa bado kuna changamoto ya ubovu wa barabara katika wilaya ya Ruangwa, serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu hiyo ikiwamo kutoa Sh. bilioni 50 kujenga barabara ya Ruangwa-Nanganga yenye urefu wa kilometa 53.3 aliyoizindua jana.

Alimshukuru pia kwa kuidhinisha kutolewa Sh. bilioni 26.5 ambazo zilielekezwa kutatua shida ya maji katika vijiji vya mkoani humo ikiwamo Narun'gombe na Nanganga pamoja na Sh. bilioni 184 za mradi mkubwa wa maji kutoka Nyangao hadi Nanganga utakaonufaisha vijiji 55.

Katika elimu alisema kwa sasa kila kata ya wilaya hiyo ina shule ya sekondari huku serikali ikiendelea kutoa pesa kujenga shule zaidi na hivi karibuni imetoa Sh. milioni 470 kujenga shule ya sekondari eneo la Michenga jambo ambalo hapo awali halikuwapo.

Alisema kwa sasa Ruangwa inapata umeme kutoka gridi ya taifa ya Dar es Salaam na vijiji vingi vinapata nishati huku Sh. bilioni 6.4 zikijenga hospitali ya wilaya, zahanati kwenye maeneo yenye shida kubwa pamoja na magari ya kubeba wagonjwa matatu.

Akizungumza na wananchi wa Mtama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema serikali inafanya juhudi kubwa kuboresha huduma za kijamii katika mkoa huo ikiwamo iliwapatia Shilingi bilioni moja kujenga na kukarabati hospitali ya Mtama iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mtama.

Alisema katika halmashauri hiyo serikali wamejenga barabara ya kilometa 24 kwa kiwango cha lami, taa za barabarani 35 na kuiagiza wizara hiyo kutoa Shilingi bilioni nne kuongeza mtandao wa barabara.

Mbunge wa Jimbo la Ndanda, Cecil Mwambe, alimwomba Rais Samia kuwapatia fedha ya kujenga hospitali katika kata ya Nanganga na ambako wakazi wake wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 100 kufuata huduma hiyo.

"Kata hii ina wakazi 16,000 lakini hatuna kituo cha afya, jengo la afya linalotumika lilijengwa mwaka 1991 likiwa na uwezo wa kuhudumia watu 3,000 tu. Sasa kata hii imekuwa kubwa zaidi hili mama tunaomba ulichukue," alisema.


SPLIT DECISIONS Company Limited

## NOTICE OF PUBLIC AUCTION

By the permission and authority given to us by the **TANZANIA AGRICULTURAL DEVELOPMENT BANK (TADB).** The following defaulters in below list, are required to pay the total amount of their remaining loan balance within twenty-one days (21) from the date of this published newspaper. Failure to do so will result into us selling by public auction the mortgaged properties as seen on the table below.

| NAME OF THE DEFAULTER | PROPERTY INFORMATION AND REGISTRATION | LOCATION | DATE AND TIME |
|---|---|---|---|
| DOMINIC MILLING GROUP LIMITED | Landed Property with Plant &Machinery in CT No 187409", LO No. 971365, Plot No 516 Block 'A' | Zegereni Industrial Area Kibaha Township | 11/10/2023 10:00 AM |
| DOMINIC MILLING GROUP LIMITED | Landed Property with Plant & Machinery in CT No 170972, LO No. 694494, Plot No 204 Block 'A' | Zegereni Industrial Area Kibaha Township | 11/10/2023 10:00 AM |
| DOMINIC MILLING GROUP LIMITED | Landed Property with Plant & Machinery in CT No 16947-MBYLR, LO No. 295853 Plot No 3 | Mponela Village. Mbozi District, Songwe Region. | 16/10/2023 10:00 AM |
| DOMINIC MILLING GROUP LIMITED | CT No 53535, LO No. 175330 Plot No 91 Block E | Msamvu Village. Morogoro Municipality | 13/10/2023 10:00 AM |

**AUCTION TERMS AND CONDITION**

- The buyer will be required to pay 25% of the total agreeable price during the auction and the remaining 75% is supposed to be paid within seven (7) days from the day of auction. The principal amount which is 25% will not be refunded if a buyer fails to pay the remaining amount within the required time.
- Inspection of the property will be made on the day of auction.
- Fee for moving the property or removing the previous tenants and changing of ownership details will be paid by the buyer.
- The property will be sold as it is.
- If anyone were to try to ruin the auction, extreme legal steps will be taken against him/her and he/she will be required to pay for the auction fees.
- The authorized agents to oversee the auction is SPLIT COMPANY LIMITED and is the one responsible for giving the final say.

SPLIT 0753 000 825/ 0626 180 070/ 0747 194 000/ 0749 700 666 217606702



SPLIT DECISIONS Company Limited

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **TANZANIA DEVELOPMENT BANK (TIB),** mdaiwa afuatae atatakiwa kulipa deni lake lote ndani ya siku kumi na nne (14) kutokea tarehe ya kutoka kwa tangazo hili. kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kuuzwa kwa njia ya mnada mali alizoziweka kama dhamana.

| JINA LA MDAIWA | MAELEZO KUHUSU DHAMANA PAMOJA NA USAJILI | ENEO | DATE AND TIME |
|---|---|---|---|
| MSK REFINERIES LIMITED | KIWANDA CHA KUCHAKA MAFUTA PAMOJA NA MASHINE ZAKE KILICHOPO KATIKA KIWANJA NAMBA 82, KITALU "A". | NYASHISHI USAGARA TRAINING CENTER KATIKA KATA YA MISUNGWI | 04/10/2023 10:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na asilimia 75% atatakiwa kumaliza ndani ya siku saba endapo atashindwa kulipa kwa muda huo uliowekwa ,pesa aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.
2. Ukaguzi wa mnada utafanyika siku ya mnada.
3. Gharama za kuhamisha mali au kumtoa mtu ndani pamoja na kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
5. Endapo yeyote atajitokeza kuharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kulazimika kulipa gharama za mnada.
6. Dalali wa mnada ni Nkaya Company Limited ndio wenye mamlaka na maamuzi ya mwisho ya kumtangaza mshindi.

SPLIT 0753 000 825/ 0626 180 070 217606702

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (kushoto), akimsikiliza Wakili wa Serikali wa Wizara hiyo, Lilian Kilembe (kulia), alipotembelea banda la wizara hiyo kwenye uzinduzi wa kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia iliyozinduliwa jana Mjini Bariadi mkoani Simiyu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 200,000 wanufaika msaada kisheria wa Rais Samia

**Na Ibrahim Joseph,** SIMIYU

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, amesema jumla ya wananchi 280,954 wa mikoa minne wamenufaika na kampeni ya msaada wa huduma ya kisheria ijulikanayo 'Mama Samia' iliyoanza Aprili, mwaka huu.

Alisema hayo jana wakati akizindua rasmi kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria kwa Mkoa wa Simiyu iliyofanyika katika mji wa Bariadi.

"Hadi sasa wananchi 280,954 wamefikiwa na kampeni hii ambayo wanawake ni 149,934 na wanaume 139,020 katika mikoa tuliyozindua kampeni," alisema.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Ruvuma, Shinyanga, Dodoma na Manyara, huku Simiyu ikiwa imefikiwa na kampeni hiyo sasa. Pia kampeni hiyo imesaidia kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaotafuta huduma za msaada wa kisheria katika maeneo yao kupitia uwakilishi mahakamani, ushauri wa kisheria na utatuzi wa migogoro.

Kadhalika, alisema kampeni hiyo imesaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuwa wananchi wamepata uelewa wa masuala ya haki za binadamu na ulinzi wa makundi maalum na kuibuliwa kwa migogoro ya muda mrefu.

Kampeni hiyo imesaidia kutatuliwa malalamiko kwa njia mbadala na kuimarisha amani kati ya pande zote zilizokuwa na migogoro.

Katika maeneo ya vizuizi, kampeni hiyo imesaidia wafungwa na mahabusu kupata uelewa wa haki zao na wapo waliopata dhamana na rufani zao kusikilizwa na hatimaye wapo waliachiwa baada ya kupata huduma za msaada wa kisheria.

Alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Simiyu na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi, ili wanufaike na msaada wa kisheria ambao unatolewa bila gharama kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa fedha za kuwawezesha wataalamu kutoa huduma hiyo bila malipo kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu. Dk. Yahaya Nawanda, alisema mkoa ukabiliwa na tatizo kubwa la maji, lakini serikali imetoa Sh. bilioni 144 kwa ajili ya mradi wa maji kwa mkoa huo.

Dk. Nwanda alisema wananchi wamehamasika mjini na vijijini, kupata huduma ya msaada wa kisheria.

Alisema wamejitokeza kwenye eneo la uzinduzi wa kampeni kupata huduma hiyo ambayo imekuwa ni tatizo kubwa kwa wananchi.

# CHADEMA yapinga tozo kwenye petroli

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeitaka serikali kuondoa tozo ya mafuta ya Sh. 100 kwa kila lita moja ya mafuta ya petroli na dizeli ili kukabili ongezeko la bei ya nishati hiyo nchini.

Kupitia kinachokiita Bunge la Wananchi la CHADEMA chini ya Spika, Suzan Lyimo na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Tito Emmanuel, chama hicho kilitoa mapendekezo hayo mkoani Dar es Salaam jana, wawili hao walipozungumza na waandishi wa habari.

Viongozi hao walisema katika kukabiliana na uhaba wa Dola za Marekani na kupanda kwa bei ya mafuta nchini, kuna haja serikali kuondoa tozo hiyo katika nishati hiyo. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Emmanuel, alisema kuna haja ya serikali kuondoa tozo hiyo haraka ili kudhibiti kuendelea kupanda bei za bidhaa na kuleta madhara katika uchumi wa nchi.

"Bunge pia linapendekeza jitihada nyingine zinazopaswa kufanyika kukabiliana na hilo ni kuongeza matumizi ya gesi viwandani na majumbani pamoja na kuongeza vituo vya kujaza gesi hiyo kutoka viwili vilivyopo sasa.

"Bunge la Wananchi linalitaka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kueleza mikakati yake ya kusambaza gesi hiyo mijini na vijijini.

"Na katika suala hili la gesi, kuna mkataba mkubwa ambao serikali iliingia na kampuni kutoka Uingereza na Norway. Ni vyema ikauweka hadharani ili wananchi tuuone na kutoa maoni yetu kuona ni namna gani gesi itasaidia katika eneo hili la nishati.

"Ni muhimu (mkataba) uwekwe wazi ili tujue nini kimo ndani. Wananchi tupate fursa ya kuuona, tujue una nini na manufaa tutakayoyapata," alisema.

Kuhusu kuadimika kwa dola, Emmanuel alisema Bunge hilo linapendekeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iweke utaratibu wa kuhifadhi vito vya thamani ili kunapotokea uhaba huo ivitumie.

Mapendekezo mengine ya chama hicho ni serikali kuwezesha wakulima kuzalisha vyakula vya msingi vya kutosheleza matumizi ya ndani na kuuza nje ya nchi na hivyo kupata dola, kuongeza mbolea ya ruzuku na kuweka ushawishi wa uwekezaji katika sekta ya kilimo.

"Hili jambo la kuagiza mazao ya msingi kama mchele, sukari na ngano kutoka nje ya Tanzania limetuletea madhara sana kwa kutumia fedha nyingi kwenda huko kuliko fedha tunayoipata kutoka nje.

"Serikali iweke mpango madhubuti wa kuhakikisha mbolea zote zinazotumika katika kilimo zizalishwe katika viwanda vya ndani na iwe iwe viwango vya kimataifa na iuzwe nje na kutuletea fedha za kigeni," alisema Emmanuel.

Vilevile, alishauri serikali ijipange kutumia bidhaa au vifaa vya ndani inapopanga kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

"Kabla ya miradi hii kuanza, serikali ilitakiwa iwe imehakikisha uzalishaji wa chuma katika nchi yetu ni wa kutosha ili kusaidia kutekeleza miradi hiyo, kwa sababu mingi huwa na uhitaji wa Dola na kuziagiza zinatumika fedha nyingi," alifafanua Emmanuel.

*SOMA HATUA ZA EWURA Uk. 4


**Tanzania Human Rights Defenders Coalition [THRDC]**

P. O. Box 105926 Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 769 642 208 E-mail: info@thrdc.or.tz
Website: www.thrdc.or.tz

**KUMB: THRDC/AGM/Vol.1/2023**

**NOTISI YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA MBILI WA WANACHAMA (THRDC)**

Kwa wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Wanachama wa Mtandao 2023.

**HII NI TAARIFA RASMI KWAMBA;** Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili (12) wa Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) utafanyika wa **siku ya Alhamisi tarehe 19 mwezi wa 10** kuanzia saa tisa alasiri mpaka saa kumi na moja jioni katika ukumbi wa **AICC** jijini **Arusha** na kwa njia ya Mtandao.

Ajenda zifuatazo zitajadiliwa:

1.1 Kuhakiki Akidi ya Mkutano Mkuu waliohudhuria
1.2 Kufungua Mkutano
1.3 Kuthibitisha na Kupitisha Ajenda
1.4 Kuidhinisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita wa mwaka 2022
1.5 Yatokanyo na Mkutano uliopita wa mwaka 2022
1.6 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya 2022
1.7 Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa ya mwaka 2022
1.8 Taarifa ya mpango kazi mwaka 2024
1.9 Ulipofikia Mchakato wa Ununuzi na Ujenzi wa Ofisi ya Mtandao
1.10 Kumpitisha mkaguzi wa nje (External Auditor) kwa ajili ya miaka 2024-2026
1.11 Kuaga wajumbe wastaafu wa bodi ya Mtandao
1.12 Kukaribisha wajumbe wapya wa bodi ya Mtandao
1.13 Hali ya Uanachama
  i. Kupitisha wanachama wapya wa mwaka 2023
  ii. Kufuta wanachama wanaodaiwa zaidi ya miaka miwili kwa mujibu wa Katiba ya Mtandao
  iii. Kuaga mratibu wa kanda ya Pemba
1.14 Kufunga Mkutano.

**NOTISI HII IMETOLEWA RASMI LEO HII TAREHE 19/09/2023.** Tunategemea kupata maoni yenu kuhusu ajenda zilizopendekezwa kabla ya tarehe 03/10/2023.
Sajili ushiriki wako kupitia barua pepe membersaffairs@thrdc.or.tz kabla ya tarehe 09/10/2023.

**Ikumbukwe kwamba, Wanachama waliokamilisha vigezo vya uanachama kama inavyoeleza Katiba ndio watakaokuwa na haki ya kuhudhuria mkutano huu. Inasisitizwa kwamba, gharama za ushiriki wa mkutano huu zitagharamiwa na mwanachama mwenyewe kwa mujibu wa katiba ya Mtandao.**

**Onesmo Olengurumwa**

**Mratibu Kitaifa**
**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**

217607902

HABARI KITAIFA

KUHODHI MAFUTA

# EWURA yafunga vituo vitatu

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imevifunga vituo vitatu kutokana na kuhodhi mafuta kwa maslahi binafsi.

Vilevile, mamlaka hiyo imeonya wamiliki wa maghala ya mafuta na wafanyabiashara wa vituo vya mafuta kupandisha bei ya nishati hiyo kiholela kinyume cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 na Sheria ya EWURA ya Mwaka 2001.

Vituo vilivyofungwa vilibainika kuhodhi mafuta katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Agosti mwaka huu. Vituo hivyo ni Camel Oil, Gairo Petrol Station chenye leseni PEL/2019/64; PETCOM, Mbalizi Petrol Station (PRL/2023/025; Rashal Petolium Ltd Mkalama (PRL/2019/034).

Mamlaka imevifunga kufanya biashara kwa kipindi cha miezi sita, lakini vimepewa muda wa siku 21 za ama kujitetea au kukata rufani.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alitangaza adhabu hiyo jana mkoani Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua wanazochukua baada ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, kutoa maagizo kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa mafuta na bei ya nishati hiyo nchini.

Alisema mifumo mitatu inarekebishwa ambayo ni uagizaji wa mafuta wa pamoja, upangaji bei na utoaji leseni.

"Sababu za upungufu wa mafuta katika baadhi ya mikoa ilhali vituo vinayo, umetokana na baadhi ya wafanyabiashara kuchukua mafuta (bandarini) na kuchelewesha kiyafikisha vituoni, huku wengine wakiwa na mafuta kwenye visima, lakini hawauzi na kusababisha kuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi.

"Kutokana na ufichaji mafuta, EWURA imechukua hatua dhidi ya vituo vinane, ambavyo vimejihusisha na tabia ya kuficha mafuta.

"Septemba 4, mwaka huu, ilivifungia vituo viwili; Camel Oil Msamvu Morogoro na Matemba. Kikao cha Bodi ya Wakurugenzi EWURA kilichofanyika Septemba 14 mwaka huu, kimetoa uamuzi huo wa kufunga vituo vitatu," alisema.

Mkurugenzi alisema serikali ilifanya sekta hiyo kuwa huria tangu miaka ya 1990 na si kuwa biashara holela, hivyo wafanyabiashara wafahamu wajibu utokanao na leseni pamoja na kutimiza haki ya huduma kwa Watanzania na si kukiuka masharti, kanuni na taratibu za leseni walizopatiwa.

Alisema EWURA inawataka wafanyabiashara katika sekta hiyo kuzingatia leseni zao na kutoa huduma hiyo. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wanaokiuka sheria.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mamlaka haitosita kufunga biashara za wamiliki wanaokiuka masharti ya leseni. Hadi sasa imeshafunga vituo vitano kwa mwezi huu pekee.


**WANATAFUTWA NA POLISI TUHUMA ZA WIZI**
**ARS/ RB: 8837/2023**



**JINA : MOSES ALFRED MABULA KABILA : MSUKUMA WA MWANZA. MAKAZI : DARAJA MBILI ARUSHA UMRI MIAKA :46**




**JINA : LAZARO RICHARD PYUZA KABILA : MNYIRAMBA MZALIWA WA MKOA WA SINGIDA MKAZI WA DARAJA MBILI ARUSHA UMRI MIAKA 37**

217604702

Watuhumiwa wa uwizi katika kampuni ya **Predators Safari Club Ltd** iliyopo Arusha maeneo ya Sakina.

***Yeyote atakayefanikisha kutoa taarifa za kukamatwa kwa watuhumiwa hawa zawadi itatolewa ya Tsh:2,000,000/=( milion mbili)***

**Kwa mawasiliano piga simu namba 0767 445344 / 0716 082447 ama toa taarifa kituo cha Polisi.**



bgtl **BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK PLC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa MNADA WA HADHARA. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.


| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MARIA OBETH MWASOMOLA | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja Na.488 kitalu 's' maeneo ya **Tabata Segerea** Migombani. **Manispaa Ya Ilala.** | 07.10.2023 | ILALA |
| 2. | YUSUPH MBOETO | Nyumba ya makazi iliyopo Mabibo Sahara yenye leseni ya makazi KND/MBB/MBO16/114 Manispaa Ya Ubungo | 07.10.2023 | ILALA |
| 3. | ALEX CHACHA AMOS | 1.Nyumba Ya Makazi Iliyopo Yombo Vituka Yenye Leseni Ya Makazi TMK/YBV/BMW25/71 Manispaa Ya Temeke. 2. Nyumba Ya Makazi Iliyopo Manzese Yenye Leseni Ya Makazi MZS/MNM/425 Manispaa Ya Ubungo. | 12.10.2023 07.10.2023 | ILALA |
| 4 | ABILAH HASSAN MATENDE | Nyumba Ya Makazi Yenye Hati Ya Mauziano Iliyopo Majohe Rada Shehe Juma Mosque Manispaa Ya Ilala. | 14.10.2023 | ILALA |
| 5 | TENTONE IMAGING TECHNOLOGY/KUMBUKA DEUS NTEJA | Nyumba Ambayo Haijakamilika Iliyopo Kigogo Kati Yenye Leseni Ya Makazi KND/KGG/KSTII/82 | 18.10.2023 | ILALA |
| 6 | ZAHARA HUSSEIN | Nyumba Ya Makazi Iliyopo Kwenye Kiwanja Chenye Leseni Ya Makazi Maeneo Ya Mangaya Mbagala TMK/MBGL/MANII/269A Manispaa Ya Temeke | 21.10.2023 | MBAGALA |
| 7 | BENSON NAHUM BAREGE | 1.Nyumba Ya Makazi Yenye Kipande Cha Ardhi Na TMK/MBGL/KZG5/299 Yenye Leseni No TMK032/02 Iliyopo Kizinga Manispaa Ya Temeke 2.Nyumba Ya Makazi Yenye Kiwanja No 28 & 29 Kitalu H Leseni Na 139102 Na No 551610 Iliyopo Chamazi Manispaa Ya Ilala | 21.10.2023 25.10.2023 | B/CENTER |
| 8 | ABDUL IMANI MGENI | Nyumba Ya Makazi Iliyopo Majohe Kichangani Manispaa Ya Ilala | 28.10.2023 | G/MBOTO |
| 9 | JOSEFINS FIDELIS WILLIAM | Nyumba Ya Makazi Iliyopo Kitunda Shule Manispaa Ya Ilala | 28.10.2023 | B/HOUSE |
| 10 | GELAS JANSON JAMES | Nyumba Ya Makazi Iliyopo Kunduchi Mtongani Manispaa Ya Kinondoni | 01.11.2023 | TEGETA |


**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

217605802


# Wafanyabiashara kizimbani kutakatisha bilioni 14/- za UDA

**Na Grace Gurisha**

WAFANYABIASHARA wamependishwa kizimbani wakikabiliwa na mashtaka matatu, likiwamo la kutakatisha Sh. bilioni 14 na kulisababishia hasara Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

Washtakiwa hao ni Saimon Bulenganija (43), William Kisena (44) na Leonard Lubuye. Walifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam na kusomewa mashtaka yao.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Fatuma Waziri alidai katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanadaiwa Oktoba Mosi, 2011 walighushi mkataba wa uongo.

Alidai kuwa nyaraka hiyo ya uongo ilikuwa ya kukodisha eneo baina ya UDA na Kampuni ya Simon Group Limited, kwa gharama ya Sh. milioni 400 kwa mwaka ndani ya miaka 10, eneo liliko Kurasini lenye ukubwa wa ekari 13 wakati wakijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa katika shtaka la pili la utakatishaji fedha, Desemba 2018, ndani ya Jiji la Dar es Salaam, washtakiwa wote walijipatia Sh. bilioni 14 kutoka UDA wakati wakijua fedha hizo zinatokana na kosa la kughushi.

Katika shtaka la tatu la kuisababishia hasara mamlaka hiyo, Wakili Fatuma alidai washtakiwa wote Mei Mosi, 2011 na Desemba 12, 2022, kwa nia ovu, walijipatia fedha Sh. bilioni 14 na kusababisha shirika hilo kupata hasara.

Lubuye alifutiwa kesi ya awali na kuunganishwa katika kesi hiyo na kusomewa mashtaka pamoja na washtakiwa hao, baada Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha mahakamani nia ya kutokuendelea na kesi dhidi yake.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka hayo, hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

Wakili huyo alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 2 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa wote walirudishwa rumande kutokana na makosa yanayowakabili kutokuwa na dhamana.

# Waziri aagiza vigogo saba wa halmashauri kuchukuliwa hatua

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amemwelekeza Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo kuchukulia hatua za kinidhamu watumishi saba wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Nteghenjwa Hosseah, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Rais - TAMISEMI, watumishi hao wanachukuliwa hatua kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, hivyo kuzorotesha utendaji kazi wa shughuli mbalimbali za halmashauri hiyo.

Nteghenjwa alifafanua katika taarifa yake hiyo kuwa Waziri Mchengerwa amechukua uamuzi huo wakati wa ziara katika Wilaya ya Liwale ya kukagua na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Rais Samia juzi alizuru kikazo wilayani Liwale.

"Waziri Mchengerwa ameelekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa mujibu wa Kanuni ya 42 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 inayoainisha kuwashusha vyeo, kukatwa mshahara kwa asilimia 15 kwa muda usiopungua miaka mitatu pamoja na kufukuzwa kazi iwapo watabainika kufanya makosa hayo," Nteghenjwa alibainisha katika taarifa yake hiyo.

Aliwataja watumishi wanaotakiwa kuchukuliwa hatua hizo za kinidhamu ni Sisty Njau, Kaimu Mhandisi wa Wilaya; Damasi Mumwi, Mkuu wa Idara ya Maliasili; Mustafa Magembe, Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika; Vinsent Moyo, Mkuu wa Idara ya Ugavi na Ununuzi; Mohamedi Songolo, Mkuu wa Idara ya TEHAMA; Sadick Bakari Khatibu, Katibu wa Afya na Tunu Mtamaha, Ofisa Ugavi na Ununuzi aliyehamishiwa Halmashauri ya Wilaya Kilwa.

"Waziri ameelekeza kuanzia sasa maofisa wote wenye kesi za rushwa na ubadhirifu wasihamishwe vituo vyao vya kazi mpaka mashauri yao yanapokamilika.

"Waziri ameagiza ofisa yeyote mwenye kesi ya uhujumu uchumi au ubadhirifu, wakati kesi yake inaendelea atakuwa anachunguza mienendo yake na hukumu yake ikitoka, hatopewa tena jukumu la ukuu wa idara au kitengo," Nteghenjwa alibainisha katika tarifa hiyo.

**TANGAZO**

# Siri kubwa Toto Afya Kadi kufanyiwa maboresho

## •Ni kuongeza msukumo wa watoto wengi zaidi kujiunga
## •Gharama zake hazijaongezeka



Kinamama wakipewa elimu ya Toto Kadi na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na dhamira njema ya serikali ya kuanzisha mpango wa Toto Afya Kadi ambapo mchango wa mtoto ulikuwa Shilingi 50,400 kwa mwaka, sawa na Shilingi 4,200 kwa mwezi na Shilingi 140 kwa siku, lakini bado lengo hilo la kufikia kundi kubwa la watoto halikufanikiwa.

Watoto wengi ambao waliandikishwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), asilimia 99 walikuwa wagonjwa na matokeo yake kupingana na dhana nzima ya bima ya afya inayotaka watu wengi wajiunge na wachache watibiwe.

Takwimu zinaonesha kuwa kundi la watoto kupitia mpango wa Toto Afya Kadi liliongezeka kutoka 24,087 mwaka 2016/17 hadi watoto 157,920 mwaka 2020/21 sawa na wastani wa usajili wa watoto 91,321, kila mwaka.

Kutokana na hali hiyo na kwa mujibu wa taarifa za NHIF, mabadiliko yaliyofanyika yamelenga kuweka msukumo wa watoto wengi zaidi kujiunga kupitia shule wanazosoma kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwa Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati ili kutimiza dhana nzima ya bima ya afya ambayo inataka watu wajiunge kwa wingi ili wachache watakaougua waweze kupata huduma za matibabu ambazo ni bora na za uhakika.

Kwa sasa utaratibu unaotumika ni watoto kujiunga kupitia shule zao ambapo tangu uanze kutumika jumla ya shule 270 zimeshajili watoto NHIF kwa kushirikiana na wazazi na jumla ya watoto 37,070 wananufaika na huduma za matibabu kwa michango ya Shilingi 50,400.

Hatua hii inalenga kuleta msukumo zaidi wa watoto kujiunga na huduma za NHIF na kwa upande wa watoto ambao hawako shuleni hao watajiunga na wazazi wao kwa gharama nafuu kupitia mpango wa vifurushi.

Takwimu zinaonesha kuwa gharama za matibabu kwa kundi la watoto zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 2.37 mwaka 2016/17 hadi Shilingi bilioni 40.58 sawa na wastani wa ongezeko la Shilingi bilioni 16.39 kwa mwaka. Uwino baina ya gharama za matibabu na michango inayokusanywa kupitia kundi hilo umeongezeka kutoka asilimia 359 mwaka 2016/17 hadi asilimia 677 mwaka 2020/21.

Uchambuzi wa gharama za matibabu kwa kundi la watoto kupitia Toto Afya Kadi, unaonesha kuwa gharama kubwa hutumiwa na kundi hilo kutokana na ada ya kuwaona madaktari bingwa (Specialist Consultation), gharama za kulazwa katika wodi ya kawaida (General Ward) na Wodi za Wagonjwa Mahututi (ICU) pamoja na gharama za upasuaji maalum.

Kutokana na mwenendo huu, gharama za matibabu kwa kundi hilo ziliendelea kuongezeka kwa kasi kubwa ikilinganishwa na michango yao. Aidha, pamoja na jitihada za Mfuko za kushawishi wananchi kuandikisha watoto wao kupitia shule, bado wananchi waliendelea kuandikisha watoto wao kwa utaratibu wa mtoto mmoja mmoja badala ya kuandikishwa watoto shuleni (group enrollment) yaani uandikishaji katika makundi.

Hali hii pia ilichangiwa na ushawishi kutoka kwa watoa huduma za afya baada ya kubaini kuwa gharama za matibabu kwa utaratibu wa malipo ya fedha taslimu hauwezekani hivyo kuwataka wazazi au walezi kukata bima ya afya kwa mtoto mgonjwa. Vilevile, uzoefu unaonesha kuwa, kuna baadhi ya wadau au taasisi zimekuwa na utamaduni wa kuwakatia bima za afya makundi ya watoto ambao tayari wana changamoto za kiafya hali ambayo ni kinyume na dhana na misingi ya bima ya afya.

Ili kuhakikisha uhai na uendelevu wa Mfuko unakuwapo, NHIF imelazimika kufanya maboresho kwa lengo la kuhamasisha wananchi wengi zaidi wajiunge ili kulinda uhai wa Mfuko, lakini pia familia au kaya ziwe na uhakika wa kupata huduma za matibabu.

Hoja ya kuwa watoto wameondolewa, siyo kweli kutokana na ukweli kwamba, NHIF imeweka mazingira rafiki ya watoto kujiunga na wazazi wao ama watoto hao kujiunga kupitia shule wanazosoma.

Je katika haya, ni NHIF ndiye mwenye makosa au ni wananchi kukubali kutumia fursa hiyo ili watoto wakatiwe bima ya afya na waweze kunufaika na huduma za matibabu na hatimaye kuondokana na malalamiko?

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unafafanua kuwa siyo kweli kuwa gharama zilizowekwa na NHIF ni kubwa bali ni hoja isiyokuwa na mashiko kwa kuwa kiasi cha Shilingi 312,000 kwa mwaka kwa mzazi na mwanawe ni sawa na Shilingi 26,000 kwa mwezi, Shilingi 6,500 kwa wiki na Shilingi 216 kwa siku.

NHIF inasisitiza kuwa ni suala la vipaumbele ambavyo mwananchi anachagua kuweka bando la simu la Shilingi 1,000 kwa siku na kwa mwezi ni Shilingi 30,000 ambayo ni kubwa zaidi kuliko kujiwekea uhakika wa matibabu.

"Katika hili tunaionea sana NHIF, kila mwananchi atimize wajibu wake kwa kuwa tayari serikali imeweka mazingira wezeshi kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya."



Baadhi ya watoto waliofaidika na Toto Kadi. **PICHA: MAKTABA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mila potofu ziepukwe kuwalinda watoto

**KUNA** baadhi ya makabila nchini bado yanaendelea kutekeleza mila ambazo zinawafanya mabinti kushawishika kuingia kwenye mahusiano ya mapenzi mapema na matokeo yake kushindwa kufikia ndoto au malengo waliyojiwekea.

Mila hizo zinaendelea kufanywa na baadhi ya makabila kama kuendeleza mila hizo zisipotee, lakini pia kuwafundisha watoto tabia njema wanapokwenda kwenye maisha ya kujitegemea au wanapokuwa wamepata wenza wao.

Mila hizo pia zinawalenga watoto wa kiume na hujulikana kama jando na unyago ambapo watoto hao wa kiume hufundishwa ujasiri na ukakamavu.

Lakini baadhi ya makabila yamekwenda mbali zaidi kwa kuwafundisha watoto wa kike jinsi ya kuishi na mume na mambo mengine ya kikubwa ambayo yanamshiwishi mtoto huyo kuamua kwenda kuishi maisha ya ndoa.

Mikoa ambayo inaonesha kuendekeza mila hizo ni ya Kusini ambako hivi sasa Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya ziara na kupata malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazazi kutokana na mila hizo.

Baadhi ya wananchi waliomba serikali kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wa kike ili kuwaepusha na ndoa za utotoni.

Pia Rais alifahamishwa kuwa tatizo hilo huibuka kipindi cha mavuno wakati wakulima wanapouza mazao yao na kuwa na fedha na baadhi ya wanaume kuamua kuongeza wake wawili na hukimbilia watoto.

Taarifa nyingi alizozipata ni kuwa katika kipindi hicho cha mavuno, wazazi huamua kutumia fedha hizo kuwacheza ngoma watoto wao ambao wengi huwa na umri mdogo, lakini hupata mafunzo ya kiutu uzima.

Imegundulika kuwa kuna wazazi wengine wakishawacheza ngoma watoto wao huwapa ruhusa ya kwenda kutekeleza kile walichofundishwa kwenye unyago na matokeo yake huishia kupata mimba za utotoni na kushindwa kuendelea na masomo.

Wazazi hao wameonywa kuacha tabia hiyo na kwamba haiwajengei mazingira mazuri watoto wa kike.

Rais aliwataka wazazi kama wanataka kuwafunza watoto wao basi wawacheze wakiwa kwenye umri ambao wanaelewa mafunzo hayo na kuchuja kipi kizuri na kipi sio kizuri kukifanya hasa wanapokuwa bado ni wanafunzi wanaohitaji kutimiza ndoto zao.

Wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wamepewa kazi ya kusimamia suala hilo ili litokomezwe kabisa ili kukabiliana na mimba za utotoni na mabinti waelekeze nguvu kwenye mambo ya msingi ikiwamo elimu.


Serikali inapojitahidi kuboresha kilimo maana yake inataka nchi iwe na ziada ya chakula na hatimaye iweze kuuza nchi za nje na nchi kupata fedha za kigeni.

Hata hivyo, kazi hiyo inayofanywa na serikali isiwe ya kuwanufaisha watu wachache kwa kufanya mambo yasiyokuwa na msingi kwa kutumia fedha wanazopata kwenye mazao waliyozalisha kwa wingine kuwacheza ngoma mabinti au wanaume kuamua kuoa wake zaidi ya mmoja.

Wengine wanashindwa hata kufanya maendeleo yao kwa kujenga nyumba bora na za kisasa, lakini wanaendelea kuishi nyumba za matope zilizoezekwa kwa nyasi huku hela zikiteketea kwa kuonyesha ufahari usiokuwa na tija.

Ushauri uliotolewa na Rais Samia ni lazima uzingatiwe wa kuachana na mila potofu. Haikatazwi kudumisha mila lakini kuwe na mafundisho yatakayomfanya mtoto wa kike kuboresha maisha yake kielimu na kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# NIT ni shangwe kwa wasichana

**MOJA** ya mbinu ambazo zinatumiwa na serikali na wadau wa elimu ili kupata wataalam wengi wanawake wa kwenye fani mbalimbali, ni kuhamasisha wasichana kupenda masomo ya sayansi lakini pia kutoa vivutio.

Motisha hiyo ni pamoja na ufadhili maalumu kwa wasichana pia kuwajengea shule za vipaji maalum na hivi karibuni jitihada hizo za kuhamasisha masomo ya sayansi kwa wasichana zikiendelea, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), nacho kinakuja na mkakati wa kuzalisha wahandisi wengi wenye weledi, hasa wanawake.

Kwa mujibu wa Naibu Mkuu wa chuo hicho anayeshugulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri, Dk. Prosper Mgaya, kupitia Mradi wa Benki ya Dunia wa Ujuzi wa Afrika Mashariki kwa Mabadiliko na Ushirikiano wa Kikanda (EASTRIP), NIT imeanzisha programu ya Ufadhili wa Ubora wa Usafirishaji (TES) ili kuweza kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike na kuzalisha wahandisi wengi zaidi katika eneo la sekta ya anga.

Dk. Mgaya anasema wameanzisha ufadhili huo, ili kusaidia wanafunzi wa kike wanaotaka kusoma programu za uhandisi wa ndege, kwa kuwa taifa lina uhaba wa wahandisi wa kike hasa katika sekta ya anga, na kwamba programu hiyo itaongeza idadi ya wahandisi wanawake katika eneo la matengenezo ya ndege.

Katika ufadhili huo, inaelezwa kuwa vigezo si tu ufaulu wa msichana utamwezesha kupata nafasi, bali vigezo vya msingi vya kutoa ufadhili huo ni kuona wasichana kutoka familia maskini na hata familia za wakulima, wananufaika na ufadhili huo wa masomo.

Aidha, anasema katika kuhakikisha wanawake wengi wanasoma masomo ya sayansi, hivi karibuni walitembelea shule za sekondari za mikoa ya Mtwara na Lindi ili kuhamasisha wanafunzi wa kike wa eneo hilo kusoma masomo hayo.

Wanastahili pongezi kwani ni kweli kwamba wengi wamekuwa wakikwepa na kukata tamaa huku wakidai kuwa masomo hayo kuwa ni magumu, hawawezi kuhangaika.

> **Kwa mujibu wa Rais wa Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET), Gemma Modu, hadi sasa, wahandisi waliosajiliwa ni 35,000, huku wanawake wakiwa ni 4,000 hali ambayo si sahihi.**

Katikati ya mazingira hayo ya kukata tamaa, bado jitihada zimeendelea kuwahamasisha wapende masomo, huku wazazi na walezi wakishiriki ili idadi ya wahandisi na wanasayansi wanawake iongezeke.

Kwa mujibu wa Rais wa Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET), Gemma Modu, hadi sasa, wahandisi waliosajiliwa ni 35,000, huku wanawake wakiwa ni 4,000 hali ambayo si sahihi.

Takwimu hizo zinaonyesha wazi kuwa zinahitajika nguvu zaidi za kuendelea kuwahamasisha wasichana kusoma kwa bidii masomo ya sayansi ili kutengeneza usawa katika taaluma mbalimbali.

Kwa kuwa hamasa kwa wanafunzi wa kike ili wapende masomo ya sayansi zinafanyika, basi ni vyema pia ukosefu wa vitendea kazi katika masomo ya sayansi ikiwamo maabara na vifaa vyake ukafanyiwa kazi.

Ninaamini hamasa ikiendelea huku shule zikiwa na vitendea kazi, dhana kwamba masomo ya sayansi ni magumu kwa wasichana, inaweza kutoweka miongoni mwa jamii ya Watanzania.

Ninadhani pamoja na mkakati huo, hamasa zaidi iendelee kutolewa ikihusisha wazazi na walezi ili wasaidie kuwahamasisha watoto wao wa kike ili wapende masomo hayo.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kupunguza pengo lililopo kati ya idadi ya wahandisi wanawake na wanaume, hatimaye kuwapo kwa idadi sawa au wanawake kuwa wengi zaidi ya wanaume.

Kwa sasa kila jambo kubwa la kihandisi likifanywa na mwanamke, jamii imekuwa ikishangaa, kwa kuwa haimani kama ana uwezo kama alivyo mhandisi wa kiume. Ninadhani idadi yao ikiongezeka, jamii haitawashangaa kwani itakuwa inajua kuwa nao wana uwezo wa kufanya mambo makubwa kama wafanyavyo wanaume.

HABARI KITAIFA

# TBS yawaita wajasiriamali kuthibitisha ubora bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wajasiriamali kujitokeza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ili wapatiwe vyeti vya ubora.

Mwishoni mwa wiki Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alitoa rai hiyo wakati wa maonesho ya wahandisi yaliyofanyika Mlimani City, Dar es Salaam.

Alisema TBS imetumia maonyesho ya 20 ya wahandisi mwaka huu kutoa elimu kwa wajasiriamali, wazalishaji wa bidhaa na wananchi wanaotumia bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa nchini.

Rhoda alisema wajasiriamali wanapaswa kujitokeza kwa wingi TBS kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha kwa kuwa huduma hiyo inatolewa bure.

Kwa mujibu wa Mayugu, wanachotakiwa ni kuwa na barua ya utambulisho kutoka SIDO na baada ya hapo shirika litaanza mchakato kuthibitisha ubora wa bidhaa zao kwa gharama zote zinalipwa na serikali.

Rhoda pia aliwataka wananchi wawe mstari wa mbele kutumia bidhaa zilizothibitishwa na TBS kwa usalama wa afya zao.

Mbali na kutoa elimu, Rhoda alisema TBS imetumia maonyesho hayo kuwataka wahandisi kuwa sehemu ya wasimamizi wa viwango.

Aliwataka wahandisi wanapokuwa katika shughuli zao za kila siku wahakikishe wanakuwa mabalozi kwa kutumia bidhaa ambazo zimethibitishwa ubora wake na TBS.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dk. James Andilile (katikati), akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Mafuta, Gerald Maganga na Meneja Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma Ewura, Titus Kagua. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# 216,000 'kutoa hukumu' uchaguzi mdogo leo

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

WAPIGAKURA 216,282 walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, wanatarajiwa kupiga kura leo uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji wa Mahakama ya Rufani Jacobs Mwambegele, alibainisha hayo jana wilayani Mbarali, mkoani Mbeya aliposoma risala kwa ajili ya uchaguzi huo na kubainisha utahusisha vituo 580 vya kupigia kura.

"Katika uchaguzi huu, kuna jumla ya wapigakura 216,282 walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura ambao watashiriki kuchagua viongozi wao. Uchaguzi huu utahusisha vituo 580 vya kupigia kura vilivyobainishwa," alisema Jaji Mwambegele.

Kata zenye uchaguzi ni; Nala iliyoko Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Mfaranyaki iliyoko Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Mwaniko iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Old Moshi Magharibi iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Marangu ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Mtyangimbole ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Mwenyekiti huyo alivikumbusha vyama vya siasa, wagombea, mawakala wa vyama, wapigakura na wananchi kuhakikisha hawapigi kampeni siku ya kupiga kura kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

"Alama za vyama vya siasa zinazoashiria kampeni kama vile vipeperushi, bendera na mavazi haviruhusiwi kutumika kesho (leo) tarehe 19 Septemba, 2023 ambayo ni siku ya uchaguzi," alionya.

Jaji Mwambegele alisema upigaji kura katika maeneo yote ya uchaguzi utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Alisema vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni.

"Iwapo wakati wa kufunga kituo watakuwapo wapigakura katika mstari ambao wamefika kabla ya saa 10:00 jioni katika mstari na hawajapiga kura, wataruhusiwa kupiga kura. Mtu yeyote hataruhusiwa kujiunga katika mstari wa wapiga kura baada ya saa 10:00 jioni," alisema.

Jaji Mwambengele alibainisha kuwa watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale tu ambao majina yao yamo katika Daftari la Kudumu la Wapigakura katika kata husika na wana kadi zao za mpigakura.

Alisema kuwa tume kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 61(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 pamoja na kifungu cha 62(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 imeruhusu wapigakura ambao wamepoteza kadi zao au kadi kuharibika kutumia vitambulisho mbadala.

"Mojawapo ya kitambulisho mbadala ambacho mpigakura anaweza kutumia ni Pasi ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)," alisema.

Mwenyekiti wa Tume pia alisisitiza kwamba ili mpigakura aruhusiwe kutumia kitambulisho mbadala, ni sharti awe ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura na jina lake limo katika orodha ya wapigakura katika kituo anachokwenda kupiga kura.

"Katika kituo cha kupigia kura, kipaumbele kitatolewa kwa wagonjwa, watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito na kinamama wanaonyonyesha watakaokwenda na watoto kituoni," alisema.

Kuhusu wapigakura kurudi nyumbani baada ya kupiga kura, Jaji Mwambegele alisema hilo ni sharti la kisheria na maadili ya uchaguzi yaliyotiwa saini na kuridhiwa na vyama vyote vya siasa, serikali na tume yanaelekeza hivyo.

"Wapigakura watatakiwa kuondoka kituoni mara wanapomaliza kupiga kura ili kuepusha msongamano na vitendo vinavyoweza kuchochea uvunjifu wa amani.

"Tume inawashauri wananchi kujiepusha na mikusanyiko katika maeneo ya vituo vya kupigia kura," alisema.

Alitoa rai kwa wapigakura katika Jimbo la Mbarali na kata sita zinazohusika na uchaguzi huo mdogo, kujitokeza kwa wingi vituo vya kupigia kura ili kuchagua viongozi wanaowataka.

Jumla ya vyama 17 vya siasa vinashiriki katika uchaguzi huo mdogo. Vyama hivyo ni AAFP, ACT-Wazalendo, ADA-TADEA, ADC, CCK, CCM, CUF, Demokrasia Makini, DP, NLD, NRA, SAU, TLP, UDP, UMD, UPDP na NCCR-Mageuzi.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# TIC yaweka rekodi kusajili miradi ya trilioni 2.3/-

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimefanikiwa kuweka rekodi ya aina yake kwa kusajili miradi 58 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 931.6 ambayo ni sawa na trilioni 2.3 ndani ya mwezi Agosti pekee.

Kwa mujibu wa taarifa ya TIC, kwenye miradi hiyo jumla ya ajira zinazotarajiwa ni 25,731 na Mkoa wa Dar es Salaam umeongoza kwa kusajili miradi 22.

Taarifa hiyo ilisema miradi hiyo 22 iliyosajiliwa jijini Dar es Salaam inathamani ya Dola za Marekani milioni 111.76 na inatarajiwa kutengeneza ajira 1,778.

Taarifa hiyo ilisema Mkoa wa Pwani umesajili miradi tisa yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 307.93 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 285.

Ilisema Mkoa wa Dodoma umesajili miradi sita yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 45.85 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 580.

Ilisema Mkoa wa Mwanza umesajili miradi mitano yenye thamani ya Dola milioni 22.41 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 440 na Mkoa wa Kagera ulisajili miradi miwili yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 226.57 ambayo itazalisha ajira 1,0120.

Kwa mujibu wa taarifa ya TIC, Mkoa wa Njombe ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola za Marekani 0.54 ambao unatarajaiwa kuzalisha ajira 30.

Mkoa wa Ruvuma ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 33.71 ambao unatarajiwa kuzalisha ajira 1,292 na Mkoa wa Morogoro ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100 ambao utazalisha ajira 1,100.

Taarifa hiyo ya TIC ilisema Mkoa wa Mtwara ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 1.07 ambao utazalisha ajira kwa watu wawili.

Ilitaja Mkoa wa Lindi ambao umesajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola za Marekani 0.98 ambao unatarajiwa kuzalisha ajira 80.

Mkoa wa Tanga ulisajili miradi miwili yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 50.50 ambayo inatarajaiwa kuzalisha ajira 411 na Mkoa wa Kilimanjaro ulisajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 8.45 ambao utazalisha ajira 182. Iliutaja Mkoa wa Arusha kuwa umefanikiwa kusajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola 0.90 ambao utazalisha ajira 30.

Taarifa hiyo ilisema Mkoa wa Mara umesajili mradi mmoja wenye thamani ya shilingi milioni 1.19 ambao utazalisha ajira 76.

Mikoa mingine ni Manyara, mradi mmoja wenye thamani ya dola za marekani milioni mbili ambao utazalisha ajira 11, Geita, mradi mmoja wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1.50 utakaozalisha ajira 54, Singida umesajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola milioni 11.25 ambao utazalisha ajira 180 wakati Mbeya imesajili mradi mmoja wenye thamani ya Dola za Marekani milioni tano na unatarajiwa kuzalisha ajira 80.

Miradi hiyo iliyosajiliwa asilimia 44 ni ya wazawa, asilimia 14 itafanyika kwa ubia (JV) wakati asilimia 42 ni ya wageni.



Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba (wa pili kulia), akitoa tuzo ya mfanyakazi wa Alliance, Henry Mgalike aliyefanya kazi miaka 20 kwenye kampuni hiyo, wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 25 toka kuanzishwa kwa kampuni hiyo, (kushoto) ni Mwenyekiti wa Alliance, Shaffin Jamal, kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Alliance, KVA Krishnan, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wazazi watakiwa kushirikisha watoto biashara wanazofanya

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ILI kukabiliana na vikwazo vya ajira pamoja na kupambana na hali duni za maisha, wazazi wamekumbushwa kuwashirikisha watoto wao biashara wanazofanya ili ziwe endelevu.

Mbunge wa Kibaha mjini, Sylvestry Koka, aliyasema hayo juzi aliposhiriki katika mahafali ya darasa la saba shule za Msingi za Kibaha Independent (KIPS), Anex na Msangani, alisema kwa kufanya hivyo ikitokea mmiliki akafariki biashara zitakuwa endelevu na ajira zitaendelea kutolewa.

"Utasikia huyu tajiri ameondoka na mali zake, hapo ni baada ya mmiliki kufariki hakuna sehemu mtu anaondoka na kitu duniani hapa. Lilichotokea ni kutowashirikisha watoto unaowaacha jinsi unavyoendesha biashara yako na ukifa sasa kama kulikuwa na ajira nazo zinakata watoto wanarudi mtaani," alisema.

Katika hatua nyingine Koka alisema sekta binafsi zitaendelea kupewa ushirikiano inapohitajika kwa kuwa kazi wanazofanya ni kuisaidia serikali kutoa huduma.

"Sekta binafsi ni muhimu na haina sababu ya kupuuzwa kwani kwa hapa wanaisaidia serikali kubeba jukumu la kutoa elimu na Rais anasisitiza ushirikiano kwa mambo mengi ikiwa ni kukabiliana na vikwazo vilivyopo," alisema.

Mkurugenzi wa shule za KIPS, Msangani na Anex, Yusuph Mfinanga, aliahidi kusomesha bure wanafunzi 20 wa darasa la saba katika shule hizo watakaofaulu kwa wastani wa alama 'A' kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne katika Shule ya Sekondari Vuchama na pia atatoa Shilingi milioni tano kwa mwanafunzi kutoka shule hizo atakayeongoza kitaifa.

Meneja wa KIPS, Nuru Mfinanga alisema, wanashirikiana vizuri na serikali kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwenye sekta hiyo lengo likiwa ni kutoa elimu bora.

Vilevile, aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao kutokana na hali ya sasa ambayo dunia inaenda kasi na maendeleo ya kiteknolojia, wawasimamie waendelee kuishi kwa kufuata maadili.

Alisema kuwapo wa sekta binafsi ni moja ya sehemu wanaipunguzia mzigo serikali na pia aliwakumbusha wazazi kuwafuatilia watoto wao badala ya kuacha kazi hiyo ifanywe na mwalimu pekee huku akisisitiza ulipaji wa ada wafanye vizuri kwenye masomo yao na kuwataka walipe kwa wakati.

# Kampuni matatani kutowalipa wakulima

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, ametoa wiki moja kwa kampuni mbili za ununuzi wa tumbaku, Mkwawa na Voesdesel kuwalipa wakulima fedha zao au watachukuliwa hatua ikiwamo kuzuiwa kununua zao hilo.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wakulima wa zao hilo pamoja na pamba wilayani Kahama, baada ya kumaliza kutembelea kiwanda cha kuchakata pamba cha Chama Kikuu Cha Ushirika Kahama (KACU).

Alisema amesikitishwa kupokea kero ya wakulima wa tumbaku kudai fedha zao za mauzo hadi sasa wakati msimu ulishapita na kuzitaka kampuni hizo ifikapo Septemba 22 ziwe zimelipa wakulima fedha zao kabla ya serikali kuchukua hatua kali.

"Kampuni kama hizi ambazo zinanyanyasa wakulima zinafaa kuzuiwa kabisa kununua tumbaku tena ni kuzi black List (kuziondoa) wasipolipa fedha hizi ambazo wanadaiwa hadi kufikia Ijumaa ijayo, lazima tuwachukulie hatua suala hili siyo la kulea," alisema Mndeme.

Aliagiza pia viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika kutoka (AMCOS 12), ambao wamesababisha hasara kwenye benki pamoja na wakulima kwa kutopeleka fedha za madeni ya mkopo kwa wakati katika benki ambazo walikopa fedha za pembejeo, Takukuru ifanye uchunguzi na kuwachukulia hatua wote waliohusika na hasara hiyo.

Katika hatua nyingine Mndeme alipiga marufuku kuanzishwa kwa vyama vipya vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), bali vifufuliwe vinavyoonekana kulala.

Alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira mazuri ya kilimo na kutetea maslahi ya mkulima ili asinyanyaswe na kampuni za ununuzi wa mazao yao kwa kutowalipa fedha zao kwa wakati, huku akitoa wito kwa KACU waanzishe pia kiwanda cha kutengeneza nguo za pamba na watapewa sehemu ya eneo la Buzwagi.

Aliwataka pia wakulima wa pamba waache tabia ya kuchafua zao hilo kwa kuweka udogo, mchanga pamoja na mawe ili kuongeza uzito wa kilo, hali inayoshusha thamani ya pamba kwa kuonekana chafu, bali inapaswa iwe safi na hata bei itakuwa juu ambayo itawanufaisha na kuinuka kiuchumi.

Naye Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Abduli Ally, akisoma taarifa kwa Mkuu wa mkoa, alisema chama kina wanachama 126, kati yao 36 wanalima tumbaku, 46 pamba na 44 mazao yote mawili na kutaja baadhi ya matatizo yanayowakabili wakulima wa tumbaku ni kutolipwa fedha zao.

Nao baadhi ya wakulima wa tumbaku akiwamo Emmanuel Marco, walisema tatizo hilo la kuchelewa kulipwa fedha zao ni hasara kwa mkulima, sababu wanashindwa kufanya maandalizi mapema ya kilimo kwa msimu ujao pamoja na kukosa fedha za kuhudumia familia na kuiomba serikali ichukue hatua za haraka ili walipwe pesa zao.



# RC apongeza vijana kuajiriwa, uchangiaji shughuli za kijamii

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amesema ameridhishwa na uchangiaji wa shughuli za kijamii na utoaji ajira 300 kwa vijana ili waweze kuinuka kiuchumi.

Aliyasema hayo juzi alipotembelea kiwanda cha Mati Super Brands Ltd, kuridhishwa na mwekezaji huyo mzawa.

Alisema kiwanda hicho kwa mkoa huo ni miongoni mwa walipa kodi wakubwa ambao wanaufanya mkoa kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha, alisema kutokana na mwekezaji huyo kufanya vizuri kwenye ulipaji wa kodi, kiwanda hicho kimeingizwa kwa walipaji wa kodi wakubwa wa kitaifa kwa kutambua mchango wao.

Sendiga alisema serikali mkoani humo ipo mbioni kuanzisha dawati maalum la kusikiliza vikwazo vya wawekezaji waliopo na wapya ambavyo wanakumbana navyo ili kuviondoa waweze kufanya kazi zao vizuri.

Alitumia fursa hiyo kupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kuajiri vijana wa kitanzania 300.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mati Super Brands Limited, David Mulokozi, alisema mazingira mazuri yaliyowekwa na Rais Samia Suluhu Hassan yanawawezesha kufanya kazi vizuri.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuishukru serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara.

**Aliyasema hayo juzi alipotembelea kiwanda cha Mati Super Brands Ltd, kuridhishwa na mwekezaji huyo mzawa.**

# Ushirikishwaji watoto, wanawake katika maamuzi wilayani Siha bado ni tatizo

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

HALI ya uthubutu na ujasiri wa makundi ya wanawake na watoto, kushiriki au kushirikishwa katika maamuzi kuanzia ngazi ya familia hadi jamii kwenye vijiji vya Naibili na Majengo mkoani Kilimanjaro iko chini, kiasi cha kuathiri ukuaji na ustawi wao kama jamii nyingine.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Mradi wa Uelimishaji Haki za Binadamu kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la TUSONGE CDO, Consolatha Kinabo, makundi ya wanawake wenye ulemavu, wanawake wajasiriamali, makundi ya wanawake vijana na watoto, yamejumuishwa pamoja kujadili ni vikwazo gani wanavyokutana navyo katika suala zima la rasilimali haki na fursa zilizoko ndani ya jamii.

Mashirika wenza yanayofanya kazi hiyo kwa pamoja na TUSONGE CDO, ambalo linaratibu na kusimamia mradi huo ni VOEWOF, WODEF, TAWOTEA na PARA LEGAL.

"Tumekutana nao kwa ujumla wao kuona umuhimu wa ushirikishwaji wa wanawake na watoto katika ngazi za maamuzi na hasa katika masuala yanayohusu ukuaji wa maslahi yao kama binadamu wengine. Tumeona ni kitu ambacho kinahitaji kupewa kipaumbele au kutiliwa mkazo zaidi.

"Kwa hiyo hii imekuwa fursa nzuri ya kukutana nao na kujadiliana kwa pamoja, kuona uelewa wao katika suala la ushirikishwaji wanaelewa nini? Hasa ni kwa namna gani wanaweza kushiriki kikamilifu, kwa sababu wengi wanaonyesha wana mwitikio wa kushiriki lakini ukiangalia ujasiri na uthubutu wa kushiriki katika ngazi za maamuzi, unaona kuna ushiriki haba ambao unachangia sana kutoa maamuzi ambayo hayakidhi mahitaji ya makundi yote yaliyoko ndani ya jamii.

...Imekuwa ni fursa nzuri ya kujengeana uwezo na ujasiri wa kushiriki ngazi za maamuzi pale madhara yanapotokea. Kwa sababu usiposhiriki maamuzi yanakuwa hayazingatii makundi yote, hayazingatii mahitaji yao ya msingi, hasa katika ngazi za serikali, ambako mara nyingi tunaona kunakuwa na uwakilishi wa watu ambao wanawasemea wanawake, hata makundi ya wanawake wenye ulemavu,"alisisitiza zaidi Consolatha.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la WODEF, Mch. Kusurie Massawe, alisema washirika wa utekelezaji wa mradi huo, wamelazimika kufanya mafunzo ya siku mbili yanayoshirikisha makundi ya wanawake na watoto, siku ya pili watawajumuisha watu tofauti kutoka makundi mbalimbali ya watoa maamuzi.

"Kwa mfano, mtoto anatakiwa asikilize, asikilizwe, kwa sababu nae pia ana haki ya kushirikishwa kwenye ngazi ya maamuzi. Lakini kinachotokea katika mifumo ya tamaduni, mila potofu na mifumo dume; haya makundi yamekuwa yakipewa tu maamuzi na sio kushirikishwa kufanya maamuzi,"alisema.

Mmoja wa wanawake wenye ulemavu, Sonia Shayo, alisema yeye binafsi, ni mara ya kwanza anapata elimu hiyo na amekuwa akipokea maamuzi kutoka kwa jamii au familia yake kwa sababu ya kutokujua kwamba anapaswa kushiriki katika ngazi ya maamuzi kuanzia kwenye familia hadi kwenye jamii nzima.

Wakati, mtoto Gadna Winston, alisema wanalishukuru Shirika la TUSONGE CDO na mashirika wenza, kuona umuhimu wa kuwafundisha sheria ya mtoto, haki za watoto na namna ambavyo wanapaswa kusikiliza na kusikilizwa katika ngazi ya maamuzi.




Diwani wa Kata ya Mtindiro wilayani Muheza mkoani Tanga, Mustafa Hatibu (mwenye miwani), juzi akimtwisha ndoo kichwani mkazi wa Kitongoji cha Mnazi Mmoja, Mwanakombo Mbwana, katika uzinduzi wa mradi wa maji visima viwili uliofadhiliwa na Taasisi ya Islamic Help wenye thamani ya Sh. milioni 20. Kulia ni Mratibu wa Idara ya Maji, Sabri Said na kushoto ni Nasibu Benjamini. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wananchi wamkataa mwenyekiti wakimtuhumu kuiba fedha

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WAKAZI wa Kitongoji cha Lubashi, kilichoko Kijiji cha Lumotio, Kata ya Pagwi, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, wamemkataa mwenyekiti wao wa serikali, Daud Kiongola, kwa madai ya kutafuna fedha zao za michango.


Wamesema fedha hizo wanatozwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo lakini hakuna kitu chochote kinachotekelezwa. Walitoa msimamo huo katika mkutano wa kitongoji hicho uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali kwa ajili ya kusikiliza kero zao. Akizungumzia suala hilo, Mtendaji wa Kijiji cha Lumotio, Mwajuma Makengwa alieleza kuwa Kiongola ametuhumiwa na wananchi kwenye mkutano mkuu wa kitongoji hicho uliyofanyika septemba 11 mwaka huu.

Makengwa alieleza kuwa wananchi hao walimkataa mwenyekiti huyo na kuwataka viongozi kuondoka nae na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa kuwa amepoteza sifa ya kukiongoza kitongoji hicho, sambamba na kutaka fedha zao zirejeshwe. "Baada ya mkutano huo uongozi wa Serikali ya Kijiji tulichukua hatua ya kumkamata baada ya kukiri kutofikisha michango ya wananchi hao kunakohusika. Tulimfikisha ofisi ya Kata kwa hatua zaidi" alieleza Makengwa. Hata hivyo alieleza kuwa wenyeviti wa vitongoji vya kijiji hicho walipewa jukumu na mkutano mkuu la kukusanya michango kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya kisasa na kwamba Kilongola hajawahi kuwasilisha fedha yoyote ambazo walichanga zipatazo Sh. 538,000.

"Tunaendelea kumtaka kila mwananchi aliyechangishwa fedha na Kilongola afike ofisi ya kijiji ili tuweze kupata idadi halisi ya fedha zilizokusanywa kwa ajili ya kupeleka shauri hili katika vyombo stahiki, hadi sasa watu wanaendelea kuja" alieleza Makengwa. Nae Mtendaji wa Kata hiyo, Abdallah Mngoya, alikiri kupokea malalamiko hayo sambamba na mtuhumiwa na kwamba tayari ofisi yake imeshachukua hatua za awali ikiwemo ya kumshikilia mwenyekiti huyo na kutaka arejeshe fedha zote alizozikusanya.

Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Michael John katika ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali, kusikiliza kero za wananchi pamoja na kuhamasisha ujenzi wa ofisi za kisasa za serikali za vijiji katika tarafa hiyo mara zote amekuwa akikemea ubadhilifu wa mali za umma.

Pia amekuwa akiwataka viongozi wa vijiji kujenga imani ya uadilifu, uwajibikaji na uwazi kwa wananchi.



# Waliojifungua wakosa eneo la kufulia nguo

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

WAZAZI katika Kituo cha Afya Sengerema Project, mkoani Mwanza wanakosa eneo salama kwa ajili ya kufulia nguo zao baada ya kujifungua, hivyo kuziweka hatarini afya zao na usalama wa kituo.

Kufuatia kukosekana kwa eneo hilo maalum kituoni huko, wamelazimika kuchimba shimo ambalo linasadia kumwaga maji yenye damu ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko yanayoweza kujitokeza kituoni.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Dk. Fredrick Mgalula, alibainisha hayo juzi wakati wa usafi kituoni huko.

Alisema kituo hicho hakina eneo la kufulia nguo za waliojifungua, hali inayopelekea kinamama hao kufua nguo katika eneo ambalo limechimbwa na kufukiwa kwa udongo.

Alisema wamechimba eneo hilo ili litumike kwa muda wakati wakisubiri kujengewa jengo la kufulia ili kuondokana na kadhia ya kufua na kumwaga ovyo maji yenye damu za mzazi.

Mganga Mkuu alikumbusha umuhimu wa kuvaa glovu kwa wanaofua nguo za wazazi hao ili kuwa na tahadhari na maradhi ambayo mtu anaweza akawa nayo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema, Casbert Midala, aliahidi kuliwasilisha suala hilo kwa Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri kuhakikisha kuanzia wiki hii wanaanza kujenga jengo kwa ajili ya kufulia ili kuondoa adha hiyo katika kituo hicho cha afya.

Ofisa Afya na Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Wilibert Muyumbu, alisema walichagua eneo la kituo hicho ili wawasaidie kufanya usafi na kufyeka nyasi ambazo zilikuwa zimeota kuzunguka eneo hilo kufuatia maadhimisho ya siku ya usafi duniani.

Mmoja wa wazazi kituoni hapo, Retisia John alisema wanapofua nguo zao, wanamwaga maji katika shimo ambalo limefunikwa kwa udongo kwa juu na hawaruhusiwi kumwaga maji hayo kwenye eneo lingine tofauti na hilo.

Alisema eneo hilo wanakofulia ni hatari kwa maisha yao na usalama kwa wagonjwa na wafanyakazi kwa kuwa maji yanayomwagwa eneo hilo yanatoa harufu mbaya ya damu.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (aliyevaa traksuti), akishiriki jana kufanya usafi katika Soko la Msufini lililopo Manispaa ya Singida, ikiwa ni moja ya maadhimisho ya Siku ya Usafishaji Mazingira Duniani. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# W'biashara watakiwa kupisha ukarabati stendi ya Bukoba

**Na Jenesta Jasson,**
BUKOBA

WAFANYABIASHARA na wajasiriamali katika stendi ya mabasi Manispaa ya Bukoba wametakiwa kuhama ili kupisha ukarabati wa stendi hiyo utakaofanyika kwa miezi sita.

Kauli hiyo aliitoa juzi na Meneja wa stendi hiyo, Himid Njovu pamoja na mambo mengine aliwaomba wajasiriamali kutosikiliza upotoshaji kwamba pindi ukarabati wa stendi hiyo utakapokamilika watakosa nafasi na watapewa watu wengine.

Alieleza kuwa tayari serikali imechukua takwimu za watu wanaofanya biashara katika stendi hiyo, hivyo baada ya kukamilika watapata nafasi zao na kuendelea na shughuli zao kama ilivyokuwa awali.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wajasiriamali katika stendi hiyo waliunga mkono mpango wa kuikarabati stendi hiyo na kuiomba serikali kuweka utaratibu mzuri wa kutenga stendi za muda ambako wataendelea na shughuli zao kwa muda.

Mustapha Sherenguzi ambaye ni wakala wa mabasi yaendayo mikoani alisema ukarabati huo ni muhimu kwani stendi hiyo imekuwa chakavu kwa muda mrefu na kuiomba serikali kutenga stendi mbili za muda kwa ajili ya mabasi na daladala.

Wakala mwingine wa mabasi, Juma Katoma alitoa pongezi kwa serikali kwa matengenezo ya stendi hiyo na kuunga mkono kuhama kwa ajili ya kupisha ukarabati wa stendi hiyo, lakini aliiomba serikali kutekeleza ukarabati huo unafanyika kwa muda uliopangwa.

# Utamaduni kupewa kipaumbele katika mtaala mpya wa elimu

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

MBUNGE wa Kahama, Jumanne Kishimba, amesema mtaala mpya wa elimu unaotarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni, utatoa kipaumbele katika somo la Utamaduni ambalo litafundishwa shuleni ili wanafunzi wajifunze na kutambua utamaduni wa Kitanzania wakiwa wadogo.

Kishimba aliyasema hayo juzi wakati wa mahafali ya pili ya Kituo cha Mafunzo ya Tiba Asili katika Kijiji cha Bani, Kata ya Mwalugulu Halmashauri ya Msalala, yakihudhuriwa na waganga wa kienyeji 600.

Mbunge Kishimba ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Vijana, alisema kuwa siku zote alikuwa analipigania suala hilo liingizwe katika mtaala wa elimu ili kuhakikisha wanafunzi wanajifunza utamaduni wakiwa shule ya msingi. Sasa linafanyiwa kazi, mtaala mpya utakuwa na somo hilo.

Aliwataka waganga wa jadi waliohitimu mafunzo hayo kuendeleza mila na tamaduni kwa njia sahihi na si kugombanisha jamii kwa kupiga ramli chonganishi. Serikali inatambua shughuli za dawa za kienyeji na zile zinazotokana na miti shamba.

Pia aliwataka wanapopiga ramli wakati wa matibabu yao, wasitoe majibu kwa wateja wao na badala yake watibu tatizo walilolona ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija katika jamii wanazotoka wateja wao.

**Aliomba serikali kuwapatia elimu ya sheria za tiba asili ili wasije kufanya kazi kinyume cha matakwa yake.**

Ramli chonganishi inapigwa marufuku na serikali kwa kuwa athari zake ni mbaya katika jamii. Zimekuwa zinasababisha mauaji, hasa ya wazee kwa tuhuma za ushirikiana.

Awali Mkuu wa Kituo cha Mafunzo ya Tiba asili, Nyeshi Ramadhani, alisema jumla ya waganga wa jadi 600 wamehitimu elimu hiyo. Wanatoka mikoa 18 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Aliwataka kuzingatia maadili ya kazi hiyo na kuepuka kujihusisha na vitendo vya upigaji wa ramli chonganisha ambayo serikali inapinga.

Aliomba serikali kuwapatia elimu ya sheria za tiba asili ili wasije kufanya kazi kinyume cha matakwa yake.

Vilevile, aliomba serikali kuwapatia vibali maalum vya kufanya kazi hiyo kwa kuwa wamekuwa wanakamatwa wanapokwenda nchi jirani kutibu. Baadhi ya wahitimu wametoka nchi jirani ya Kenya.

Mmoja wa wahitimu kutoka mkoani Kilimanjaro, Shafii Rajabu, alisema elimu aliyoipata itamwezesha kusaidia jamii kwa kutibu magonjwa mbalimbali na kuvutia utalii.



Ukurasa 12

Tanzania ya kidijitali program itakayoleta zama kiteknolojia



Ukurasa 13

Taulo za kike zilivyojibu kwa kupandisha taaluma

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 19, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

Alois Alzheimer; mtaalamu nguli mgunduzi wa maradhi ya usahaulifu

ELIMU

NA SALUMU MATATA, UDSM

TAIFA KINARA ULEVI

# Ije tena ‘operesheni tokomeza viroba’ kukabili ‘pepo’ kulewa kupindukia



AFYA ni tunu isiyoweza kulinganishwa na chochote, tena inayostahili kulindwa kwa juhudi zote kwani ndiyo uzima na chachu ya kumudu maisha kwa kufanyakazi hasa kwa kundi la nguvu kazi vijana na watu wazima.

Kwa taifa lolote nguvu kazi tegemeo ni vijana wanaoleta maendeleo ya nchi kwa kufanyakazi kuanzia mashambani, mijini na vijijini. Nchi isiyo na vijana ni kama imepungukiwa rasilimali muhimu.

Wiki inapoanza bado wengi waliomaliza juma na taarifa za vijana kunywa pombe kupindukia bado wanatafakari kwa kina.

Ni baada ya Wizara ya Afya kutangazia umma kuwa Tanzania inaongoza kwa ulevi Afrika ikishika namba moja huku watoto wenye miaka 15 na kuendelea wakitumia wastani wa ndoo moja ndogo kwa mwaka.

Anasema Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza (NCD) wizarani hapo, Dk. Omary Ubuguyu.

Anasema vichocheo vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ni pamoja na pombe huku akisema, mwaka 2012 asilimia 29 ya Watanzania walikuwa wanakunywa pombe na zaidi ya asilimia 24 wakiwa ni wanaume ambao hulewa kwa kiwango kikubwa.

“Kwa Tanzania ukiangalia takwimu, hata sasa inaongoza kwa matumizi ya pombe Afrika. Kwa wastani kila Mtanzania kuanzia umri wa miaka 15 kuendelea anatumia wastani wa ndoo ndogo ya pombe kwa mwaka.”

“Kwa Tanzania ukiangalia takwimu, hata juzi zilitoka kwamba, Tanzania inaongoza kwa matumizi ya pombe Afrika. Kwa wastani kila Mtanzania kuanzia umri wa miaka 15 na kuendelea anatumia wastani wa ndoo ndogo ya pombe kwa mwaka.

“Si kiwango kidogo, maana yake tunasema kwamba kwa mwaka ni kiwango cha unywaji ni lita 9.1 (sawa na ndoo ndogo ya lita 10), wakati kiwango kwa Afrika ni lita sita kwa mwaka, sisi tupo juu kwa lita 3.1 zaidi,” anasema.

Itakumbukwa mwaka 2017 wakati huo John Magufuli, akiwa madarakani serikali ilikataza na kupiga marufuku pombe za viroba ambayo ilikuwa imekithiri katika karibu kila kona ya nchi ikiwa ndani ya mifuko ya plastiki karibu kila kijana alikuwa akiifyonza.

Wapo waliokuwa wanabeba kwenye mifuko ya suruali, makoti na hata kwenye mashati. Ilifika kipindi madereva wa bodaboda, bajaji na hata mabasi ya masafa, walikuwa wakifyonza huku wakiendesha abiria na ulevi huo uliofanyika hadharani.

Wakati huo kiroba kikiuzwa Shilingi 500 kwa paketi ndogo na 1,000 kwa kikubwa, takataka za mifuko ya pombe hiyo ilikuwa imezagaa na kuchafua karibu ardhi yote ya taifa hili.

Utafiti uliofanywa na baadhi ya taasisi vikiwamo vyuo vya elimu ulibaini kuwa pombe hiyo ilikuwa inatumika hata kwa wanafunzi waliovibeba na kuviweka kwenye mabegi na mifukoni vikiwa na kiwango cha kilevi kuanzia asilimia 37 mpaka 40.

Wapo wafanyakazi waliodaiwa kuwa kabla ya kwenda kazini walipitia dukani na kununua kiroba kisha hunywa kabla ya kuingia kazini na kupelekea kutofanya kazi kwa weledi na ufanisi lakini vilipigwa marufuku hali iliyokomesha kutumia pombe kali iliyokuwa inapatikana kwa bei rahisi.

Licha ya viroba kufyekwa huenda hali imerudia kama ilivyokuwa, leo maduka yamejaa pombe kali za kila namna zinauzwa kuanzia Shilingi 2,000 na endapo kijana atakosa bei hiyo ya chupa nzima anaweza kununua nusu kwa kupimiwa ya Shilingi 500, 800 hata 1000.

Kwa kifupi kuanzia pesa kidogo unaweza kulewa kwa kupimiwa kiasi kidogo kutoka kwenye chupa kubwa ambayo inauzwa Shilingi 12, 000 na ndogo 4,000 endapo kubwa itakakosekana, ni kwa mujibu wa utafiti unaofanywa na Nipashe kwenye baa na migahawa jijini Dar es Salaam.

Vipo vioski pembeni ya barabara vinauza pombe mchana kweupe tena kuna kila aina zipo za kutoka ndani na nje ya nchi.

Kuna vipimo halisi kutegemeana na dau la mlevi, bilauri ndogo hadi kubwa hutumiwa kununua kidogo lakini hata mzinga mzima mteja akitaka, licha ya kuwa ni pombe kali na zenye vilevi vikubwa mno zaidi ya asilimia 60 ambapo vijana wengi huipenda ili walewe haraka pale wanapokosa pesa ya kununua bia zenye gharama kubwa.

Kundi hili ndilo linalotajwa na serikali kuwa ni wanywaji kupindukia, ambalo hupitia mambo mbalimbali ya kidunia na hata kuchanganyikiwa ndiyo maana kuna msemo kuwa “ujana ni nusu ya uchizi” ukimaanisha kuwa kila kitu cha kidunia na starehe vijana wanataka kuzifanya.

Katika miaka ya nyuma vijana ndio kundi kubwa lililokuwa na afya bora kutokana na kutokushiriki vilevi mbalimbali kama ilivyo sasa kwani katika miaka ya hivi karibuni wamekumbwa na changamoto mbalimbali kutokana na matumizi ya vilevi kupindukia.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Tanzania ya kidijitali programu itakayoleta zama mpya kiteknolojia

UWEKEZAJI katika sayansi, teknolojia na uvumbuzi (STI) ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya kijamii. Utafiti na maendeleo (R&D) unaweza kukuza maendeleo endelevu kwa kujenga jamii zisizo na umaskini, linasema Shirika la Elimu,Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) .

Kupata wataalamu wazawa katika sekta ya sayansi na teknolojia kunahitaji uwekezaji wa kutosha katika kuwapatia maarifa, ujuzi na stadi.

Ili kutimiza lengo hilo la kuwapata wanasayansi ili kufanya kazi katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi serikali inaanza kuchukua hatua mbalimbali,

Ukweli ni kwamba sayansi na teknolojia inahitajika zaidi katika jamii sasa na siku zijazo ili kukidhi mahitaji yanayohusisha uvumbuzi na ugunduzi wa kiteknolojia kufikia maendeleo na kutimiza malengo ya muda mfupi na mrefu ya kitaifa ya karne ya sasa na zijazo.

Ni muhimu, ili kuhakikisha usalama wa taifa na utulivu wa kijamii unaoletwa na kupata huduma bora za kijamii, kuanzia chakula na tiba vile vile kuleta ukuaji wa uchumi wa taifa na kuboresha ufanisi wake.

Hivyo, kuendeleza wataalamu hao na kuhakikisha kuwa wanaendelea kuwapo ni mikakati inayofanyika na serikali kwa sasa ikitangaza kuanza kuwasomesha vijana ili kupata wabobezi wa kutosha watakaokuwa chachu ya kuleta mageuzi, mapinduzi na maendeleo katika tasnia za sayansi na teknolojia, hivyo kuchangia jitihada za kufikia uchumia imara, jamii bora na taifa lenye maendeleo endelevu.

Tanzania ya sayansi na teknolojia itafikiwa endapo uwekezaji mkubwa na endelevu



Wasichana wakiandaliwa kuwa wataalamu wa sayansi kwenye maabara. **PICHA: MTANDAO**

utafanywa kwa vijana kwa kuwapatia maarifa, stadi na ujuzi katika nyanja hiyo ili kuchochea mabadiliko kwenye maeneo ya kilimo, tiba, ufugaji, uvuvi, uziduaji, ujenzi, kuendeleza ugunduzi na ubunifu.

Katika awamu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania) imetenga dola bilioni 4.7 kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na mafupi kwa wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) 500.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Utawala na Raslimali Watu wa Wizara hiyo, Salome Kessy, mradi huo umepanga kugharamia mafunzo kwa watumishi 500 kati ya hao 50 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu huku 450 wakipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya teknolojia.

Vilevile, katika hafla ya kuwakabidhi vyeti vya ufadhili wa masomo kwenye mradi huo wa Tanzania ya Kidijitali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohammed Khamis Abdulla,anasema:

"Nitoe rai kwa kila aliyepata ufadhili huu, kutumia kikamilifu fursa hii kujifunza kwa bidii kwa lengo la kuongeza uelewa na maarifa ili mtakaporudi muweze kuleta mabadiliko chanya yatakayosaidia kuboresha utoaji wa huduma za serikali."

Wanufaika wa ufadhili huu wanalo deni kwa taifa kwani ufadhili waliopata si kwa manufaa yao binafsi bali ni kwa manufaa ya taifa ikizingatiwa fedha zinazotumika kuwasomesha ni kodi za Watanzania. Juhudi za Tanzania kupiga hatua za kimaendeleo haziwezi kutenganishwa na matumizi ya TEHAMA.

Hivyo basi, wanufaika wa ufadhili huu wanawajibika moja kwa moja kulipa deni kwa taifa lao kwa kuhakikisha kuwa wanatumia maarifa, stadi na ujuzi watakaopata kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa manufaa ya taifa.

Ufanisi na utendaji kazi bora unachagizwa na matumizi ya TEHAMA. Watumishi wa serikali waliopata fursa ya ufadhili huu wanao wajibu wa kuhakikisha baada ya kuhitimu masomo yao; ufanisi, tija na utendajikazi unakuwa bora zaidi ili uwekezaji uliofanywa na serikali usiwe ni upotevu wa fedha.

Kwa mfano, Tanzania inahitaji wataalamu kujibu matatizo ya kilimo kwa kuwa ardhi inayotumika katika kilimo sasa imeharibika kutokana na matumizi ya viuatilifu vya viwandani, mabadiliko ya tabianchi, mbolea zenye madhara na teknolojia inayoharibu uasilia wa rasilimali hiyo. Hivyo kuhitajika zaidi wanasayansi wa kuleta ufumbuzi.

Aidha, wananachi wanaohudumiwa katika ofisi mbalimbali za umma wanategemea kupata huduma bora zenye kuokoa muda. Hivyo, wanufaika wa ufadhili wa mradi wa Tanzania ya Kidijitali wanategemewa kutoa huduma bora kwa wananchi na kutumia teknolojia katika kuwahudumia wananchi wengi na kwa muda mfupi .

Serikali inafanya juhudi kuhama kutoka utendajikazi unaotumia makaratasi na kuingia katika mifumo ya kiteknolojia. Matumizi ya teknolojia yana manufaa kwa wananchi kwani yanaokoa gharama za wananchi kufuatilia mambo yao na hivyo mwananchi anaweza kuhudumiwa akiwa nyumbani kwake. Mradi huu wa Tanzania ya Kidijitali ni nyenzo muhimu katika kufanikisha azma ya serikalini kutumia sayansi na teknolojia kuwahudumia watu wake na kuachana kabisa na matumizi ya makaratasi.

Serikali ina kazi kubwa ya kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo kusambaza vifaa vya teknolojia kama vile vishkwambi, kompyuta na kufunga mifumo ya intaneti katika taasisi za elimu kama vile shule na vyuo ili kujenga msingi bora wa kuandaa watoto na vijana wa kitanzania kutumia sayansi na teknolojia wakiwa shuleni na vyuoni ili uelewa wa matumizi ya teknolojia katika utendajikazi uanze mapema.

***Mwandishi ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0620 800 462***

## Ije tena 'operesheni tokomeza viroba' kukabili 'pepo' kulewa kupindukia

**INATOKA UK.11**

Daniel Mguvano anaishi Kijitonyama Dar es Salaam, akizungumzia utumiaji wa pombe kali anasema unaongezeka kwa sababu mbalimbali kama uhaba wa kipato unawafanya watumie ulevi kupunguza msongo wa mawazo kwa vile ukiwa na 2,000 unalewa na kuzimika.

Anasema wanapotumia pombe kali wanapata ujasiri wa kufanya jambo lolote pale wanapokutana na maudhi, kero au hata ukiwa na dukuduku moyoni na unashindwa kumwambia yeyote ukishatumia inakupa ujasiri wa kumwambia jambo hilo au hata kusema bila woga.

**KUHUSU MADHARA**

Vijana wanaozungumza na Nipashe wanasema wanajua kama pombe zina madhara ila wanajipa moyo kuwa kila kitu kina madhara katika dunia hii hivyo ukianza kufikiria madhara utaacha vyote kwani hata soda si salama zina vichocheo hatari na viambato vya kulevya.

Wanapoulizwa kwanini wengi wanatumia ulevi bila kula wanasema unapotumia pombe kali kabla ya kula chochote unakuwa huhisi njaa hivyo kunywa ni njia ya kupunguza shida zinazotokana na kushindwa kumudu kula kwa vile maisha ni magumu.

Wanasema wanaokunywa pombe kali wengi hushindia maji na chakula kidogo mno, lakini ulevi ni mbaya unaleta uraibu inaifika kipindi wanakuwa watumwa.

Vijana hawa wanashauri kuwa nguvu, juhudi na mikakati iliyotumika kumaliza ulevi wa viroba ielekezwe kukomesha ulevi kupindukia wa kunywa ndoo ndogo au lita 10 za pombe kwa mwaka ambao sasa ni kitisho kwa vijana wa taifa hili.

ELIMU

NA ELIZABETH JOHN, NJOMBE

# Taulo za kike zilivyojibu kwa kupandisha taaluma

• Wasichana juu zaidi, 'divisheni 1' tele, ziro kuwa historia

"KABLA ya kuanza kugawa taulo kwa wanafunzi wa sekondari kwenye matokeo ya mitihani ilikuwa shida kupata daraja la kwanza.

Hawakupatikana hata 50, lakini sasa kuna waliopata daraja la kwanza zaidi ya 100 na kwenye sifuri nako tunaondoka. Mfano mwaka 2019 sifuri zilikuwa 110, lakini 2022 wamekuwa 49 zimepungua karibu asilimia 50 ."

Anasema Ofisa Elimu Taaluma Sekondari Halmashauri ya Mji Njombe, Huruma Chaula, anapozungumza kwenye mahojiano na Nipashe.

Anaongeza kuwa mkakati wa kugawa taulo za kike shule za sekondari umeleta matokeo chanya na kwamba huduma hiyo imeondoa woga na kukosa vipindi kumekwisha.

Wasichana wanaotokea kwenye familia duni hushindwa kuhudhuria masomo wanapokuwa katika siku zao hivyo, kushuka kitaaluma, anasema.

Anaongeza kuwa ugumu wa maisha ni moja ya sababu inayotajwa kusababisha kushindwa kumudu gharama za kununua taulo za kike na kutumia njia zisizo salama wala kuaminika.

Halmashauri ya Mji Njombe imetekeleza agizo la serikali la kuzitaka halmashauri nchini kutenga bajeti kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa taulo za kike, ikitenga Shilingi milioni 10 kila mwaka kwa ajili ya sekondari na 5,000,000 ya shule za msingi kwa mujibu wa Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Kuruthum Sadick.

Anaongeza kuwa utekelezaji rasmi wa kugawa taulo ulianza 2021 na kuna mafanikio baada ya wanafunzi wa kike kupanda kitaaluma na kwamba mpango wa kugawa taulo hizo ni endelevu na kwamba wamefikia shule 26 za sekondari za serikali na binafsi zenye wasichana.

"Kila mwaka tunatenga bajeti ya milioni 15, kwenye fedha hiyo milioni 10 ya wanafunzi wa sekondari na milioni tano kwa shule za msingi, hapo awali watoto wa kike walikuwa wanashindwa kuhudhuria masomo kutokana na hedhi leo habari inabadilika," anasema Kuruthum.

Baadhi ya wanafunzi wa sekondari Mabatini, Mpechi na Viziwi zote za Halmashauri ya




Wafanyakazi wa Televisheni ya EATV wakiwa katika juhudi za kusaidia upatikanaji taulo za kike kitaifa. **PICHA: EATV**

Mji wa Njombe, wanasema hali hiyo ya kimaumbile iliwakwamisha kutokana na kukosa vifaa vya kujisitiri, anasema Lusiana Mgani wa Mpechi.

Laitnes Mtega kutoka Sekondari Mabatini anaishukuru serikali na Halmashauri ya Mji kwa kuwapatia taulo ambazo zinawaongezea ari ya kusoma kwa bidii na kufaulu zaidi.

**HALI HALISI**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) linasema kwa wastani wasichana wanaripotiwa kushindwa kuhudhuria masomo kwa siku tatu hadi tano kwa mwezi ikiwa ni siku 36 hadi 60 mwaka hali inayochangia kutofanya vizuri masomoni.

Dunia inakusudia kwamba ikifika mwaka 2030 iwe imetekeleza malengo 17 ya maendeleo endelevu ambayo miongoni mwao ni lengo namba tatu linalojikita katika afya na ustawi bora wa kila mtu. UNFPA inasema mamilioni ya watoto wa kike, wasichana na wanawake duniani, mzunguko wa hedhi ambao ni jambo la kawaida umegeuzwa kuwa chanzo cha ndoa za umri mdogo pale binti anapobalehe.

Aidha, ukatili wa kingono, unyanyapaa, mtoto kukosa shule hata kuchukuliwa kuwa ni chanzo cha aibu pale anapochafua nguo akiwa shuleni kwa sababu ya jamii kutofahamu umuhimu wa hali hiyo ya maumbile ambayo ni sehemu ya michakato ya uzazi.

Siku za hivi karibuni baadhi ya nchi zimepitisha taulo za kike kuwa ni bure au kuondolewa kodi na ushuru kama njia ya kutokomeza umaskini unaotokana na kukosekana kwa mkakati wa hedhi salama, linaongeza shirika hilo na kuunga mkono haki ya afya ya uzazi kwa kila mtoto na kusisitiza kuwa ni lazima kuzingatia hedhi bila kunyanyapaliwa au kutengwa au kuhisi kuwa ni aibu.

Utafiti wa mwaka 2015 wa Shirika la Netherlands Development (SNV), pamoja na Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET) katika halmashauri za Sengerema, Mufindi, Chato na Temeke ulibaini kuwa asilimia 48 ya wanafunzi wasichana hukosa masomo wanapokua kwenye hedhi. Kiasi kingine cha asilimia 78 waliohojiwa walisema kipindi cha hedhi huathiri uwezo wa kujifunza.

Aidha, taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kuhusu masuala ya maji na usafi wa mazingira shuleni ya mwaka 2018, inaonyesha kuwa asilimia 66.8 ya shule ndizo zinahuduma ya hedhi salama na kwamba kati ya hizo, zilizobainika kuwa na viteketezi ni asilimia 24 huku asilimia 22.8 zikibainika kutupa taka kwenye mashimo na asilimia 19.5 zinavichomea taka visivyokidhi viwango.

> Takwimu zinaonyesha kuwa wanawake takribani milioni 13.7 wenye umri wa miaka 15 hadi 49 hupata hedhi kila mwaka.

Matokeo ya utafiti uliofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu NIMR pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI) kwa kushirikiana na wadau wa hedhi salama mwaka 2019, inaonyesha changamoto nyingi ziko kwenye ngazi ya jamii kutokana na uelewa mdogo.

Akiwa katika maadhimisho ya siku ya hedhi hivi karibuni jijini Dodoma, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, anasema takwimu zinaonyesha kuwa wanawake takribani milioni 13.7 wenye umri wa miaka 15 hadi 49 hupata hedhi kila mwaka.

Idadi hiyo ni kubwa, hivyo jamii ina kila sababu ya kuhakikisha kuwa kundi hilo linapata huduma bora wakati wa hedhi ikiwamo maji, sabuni na taulo za kike ili kuifanya hedhi iwe salama.

Mwitikio wa hedhi salama kwa wanaume au ushiriki wa o unaelezwa kuwa una pande mbili, baadhi wanaunga mkono kwa kueleza kuwa suala hilo ni la siri (binafsi) ambalo husababisha hata ugumu kwenye mkakati wa upatikanaji wa taulo za kike.

Licha ya kuwapo kwa changamoto hiyo, wapo baadhi ya wanaume wanaizungumzia hedhi kama ni maumbile tu, kama anavyoeleza Festo John kuwa tamaduni zinachangia kwa sababu wanaume wanaona kama si kitu cha kawaida.

"Jinsi mila zetu zilivyo mtu anaishi hajui ashiriki vipi. Kwanza tunafikiria hili suala halituhusu," anasema John mkazi wa Njombe na kwamba ili kuondoa mkanganyiko huo wazazi wa kike waache kuwajengea woga mabinti kuwa suala hilo linawahusu wao pekee.

"Dhana imejengeka kwamba suala la hedhi ni la wanawake tu, lakini na sisi linatuhusu, tuache tamaduni za zamani, hata utaratibu wa taulo za kike uwe ni kawaida ziwepo ndani au hata baba aone ni kawaida kumnunulia binti yake isiwe ajabu," anafafanua John.

Jafari Nziku, anasema wanaume hawapo sana kwenye suala la hedhi kwa sababu wameachwa nyuma na hawashirikishwi, katika hatua hiyo anapongeza maamuzi yaliyochukuliwa na taifa na kutekelezwa na Halmashauri ya Mji Njombe kuwa ni ya kuingwa kwa sababu ni ushirikishwaji.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Alois Alzheimer; mtaalamu nguli mgunduzi wa maradhi ya usahaulifu

KUSAHAU ni tatizo linaloathiri mamilioni ya watu duniani leo na pengine unaweza kupewa jina maradhi ya usahaulifu. Ambayo kitaalamu huitwa 'Alzheimers'.

Pengine umesikia neno "Alzheimers" au ugonjwa wa kusahau, mara nyingi katika maisha haya, lakini kuna uwezekano kwamba unajua kidogo au hujui chochote kuhusu daktari ambaye aliigundua na kuupa ugonjwa huo jina lake.

Alois Alzheimer, ndiye mgunduzi, aliyezaliwa Juni 14, 1864 katika kijiji kidogo cha jimbo la Ujerumani la Bavaria, alianza masomo yake ya matibabu huko Berlin, mji mkuu wa Ujerumani, kwa ombi la wazi la baba yake.

Aliamua kurudi katika mji wake ili kukamilisha masomo yake katika Chuo Kikuu cha Würzburg mwaka wa 1887.

Tangu wakati huo, alijitolea kuchunguza na kufuatilia magonjwa ya 'neuropathology' na utafiti wa magonjwa ya akili.

Muda mfupi baada ya kupata diploma yake, akiwa na umri wa miaka 23, aliajiriwa kama daktari binafsi kwa mwanamke aliyekuwa na matatizo ya akili.

Alikuwa akisafiri naye kwa miezi mitano, kufuatilia kwa karibu na kutazama mabadiliko ya shida zake.

Baada ya uzoefu huu, aliajiriwa na manispaa kushughulikia watu wenye matatizo ya akili na kifafa katika jiji la Frankfurt, Ujerumani.

Mwanzoni mwa miaka ya 1900, daktari Alzheimer alipata wazo kwamba magonjwa ya akili yalikuwa kama maradhi mengine, Conrad Maurer, profesa aliyestaafu wa magonjwa ya akili katika Chuo Kikuu cha Goethe huko Frankfurt, anaiambia BBC.

Anasema alifikiri kwamba "kama kulikuwa na magonjwa ya mwili, pia kulikuwa na maradhi ya ubongo". Profesa Maurer, daktari wa magonjwa ya akili alidhamiria kutafuta mgonjwa ili kuthibitisha hilo, anasema.

Wakati huo ndipo alipokutana na Auguste Deter ambaye kutoka mwaka 1901, alipoteza kumbukumbu, alikuwa na wasiwasi na kupiga kelele au kulia hata katikati ya usiku.

Alipomwona, Dokta Alzheimer alijisemea "hii ni kesi yangu", anasema Maurer. Daktari huyo alifungua jalada la matibabu kwa ajili ya Deter ambalo lilipatikana katika miaka ya 1990 na timu ya Maurer, mkurugenzi wa hospitali ya magonjwa ya akili ambapo dokta Alzheimers alifanya kazi.



Dk. Alois Alzheimers mgunduzi wa ugonjwa wa usahaulifu. **PICHA: MTANDAO**

> Ingawa saratani ya matiti inatambuliwa kihalali kama shida ya kiafya ya wanawake, ugonjwa wa Alzheimer hautambuliwi.

"Ninamwonyesha penseli, kalamu, mkoba, funguo, shajara na sigara na anazitambua kwa usahihi," alisema. "Nilipomtaka aandike jina lake Auguste Deter, anaandika mume na kisha tunalazimika kurudia maneno mengine kwa sababu anayasahau. Kuendelea katika uandishi wake na kurudia rudia" yote hayo yakionyesha jinsi gani alivyoathirika na kusahau.

Kwa mujibu wa Maurer, mara tu baada ya kifo chake, ubongo wa Auguste Deter, ulichambuliwa kikamilifu na mtaalamu wa magonjwa ya akili.

Ugonjwa wa Alzheimer ulitokeza alama nyingi ambazo bado zinaweza kuchunguzwa hadi sasa na kipengele muhimu zaidi ambacho daktari wa akili alipata katika ubongo wa Augustus kwamba cortex ya ubongo ambayo ni sehemu ya nje ya ubongo yenye tishu za seli za neva, ilikuwa nyembamba mno kwa kusinyaa.

Pia aligundua mkusanyiko wa plaques ambazo ni protini, zilizojijenga kati ya seli za neva za ubongo, ambazo zilielezea ugonjwa wake.

Hata leo, "tunadhani hiyo ndiyo sababu ya ugonjwa," Profesa Maurer anasema.

Takribani miezi sita baada ya kifo cha Auguste, Alzheimer alitoa mada muhimu katika mkutano wa 37 wa kisaikolojia wa Ujerumani Kusini, akielezea mwendo wa kupungua kwake kiakili, dalili za neva, pamoja na changamoto zake daktari huyo alifariki mwaka wa 1915, akiwa na umri wa miaka 51, bila kujua kwamba ugonjwa wa Auguste siku moja ungeathiri maisha ya mamilioni ya watu na kusababisha jitihada kubwa za utafiti wa kimataifa.

Wanasayansi wanamtaja sio tu mgunduzi wa ugonjwa wa neurodegenerative, au uchakavu wa mishipa ya ubongo lakini pia njia ya ubunifu ya utafiti, kwani utambuzi wa ugonjwa wa shida ya akili bado unategemea njia sawa za utafiti kama zile zilizotumiwa miaka ya 1906.

**KINAMAMA HATARINI**

Ripoti za BBC zinasema kuwa matatizo mbalimbali ya neva na akili huathiri wanaume na wanawake kwa viwango tofauti na kwa uwiano usiofanana pia.

Utafiti unaonyesha kuwa ubongo wa wanaume na wanawake huzeeka tofauti, kwa mfano, wanawake wana uwezekano mara mbili ya wanaume kugunduliwa kuwa na matatizo ya wasiwasi au mfadhaiko na uwezekano mara tatu wa kupata matatizo ya kinga ya mwili ambayo huathiri ubongo, kama vile sclerosis nyingi.

Aidha, wanawake wana uwezekano mara nne zaidi wa kuteseka na maumivu ya kichwa na kipandauso kuliko wanaume.

Aidha, wana uwezekano mkubwa wa kupata 'meningiomas' aina ya uvimbe wa ubongo, na wana uwezekano mkubwa wa kupata kiharusi hatari.

Ndiyo huathirika zaidi na ugonjwa wa Alzheimer kisababishi kikuu cha shida ya akili duniani kote, ambayo huathiri zaidi ya watu milioni 35.

Karibu wagonjwa wawili kati ya watatu wenye Alzheimer ni wanawake, ikimaanisha kwamba kwa kila mwanaume mwenye ugonjwa wa Alzheimer, kuna wanawake wawili.

Hivi sasa, tunapozungumzia "afya ya wanawake", ni afya ya uzazi ambayo tunazungumzia. Ili kutoa wazo, mwanamke mwenye umri wa miaka sitini ana uwezekano wa karibu mara mbili wa kupata ugonjwa wa Alzheimer baadaye maishani kuliko kupata saratani ya matiti.

Ingawa saratani ya matiti inatambuliwa kihalali kama shida ya kiafya ya wanawake, ugonjwa wa Alzheimer hautambuliwi.

Hadi leo, afya ya ubongo wa wanawake inabakia kuwa maeneo ambayo hayajachunguzwa kikamilifu, yasiyotibiwa na yanayopatiwa ufadhili kidogo, hivyo ni muhimu kushughulikia tofauti hii na kupanua wigo wa afya ya wanawake ili kujumuisha masuala haya muhimu.

Zaidi ya hayo, wanawake wana uwezekano mara nne zaidi wa kuteseka na maumivu ya kichwa na kipandauso.

Wanawake pia wana uwezekano mkubwa wa kupata meningiomas, aina ya uvimbe wa ubongo, na wana uwezekano mkubwa wa kupata kiharusi hatari. Wanawake huathirika zaidi na ugonjwa wa Alzeima, kisababishi kikuu cha shida ya akili ulimwenguni kote, ambayo huathiri zaidi ya watu milioni 35.

Kwa kushangaza, karibu wagonjwa wawili kati ya watatu wenye ugonjwa wa Alzheimer ni wanawake, ambayo ina maana kwamba kwa kila mwanaume mwenye ugonjwa wa Alzheimer, kuna wanawake wawili.

Licha ya takwimu hizi, hakuna magonjwa haya ambayo yameainishwa kama "afya ya wanawake".

Hivi sasa, tunapozungumzia "afya ya wanawake", ni afya ya uzazi ambayo tunazungumzia. Ili kutoa wazo, mwanamke mwenye umri wa miaka 60 ana uwezekano wa karibu mara mbili wa kupata ugonjwa wa Alzheimer baadaye maishani kuliko kupata saratani ya matiti.

Ingawa saratani ya matiti inatambuliwa kihalali kama shida ya kiafya ya wanawake, ugonjwa wa Alzheimer hautambuliwi.

Hadi leo, afya ya ubongo wa wanawake inabakia kuwa mojawapo ya maeneo ambayo hayajasomewa, ambayo hayajachunguzwa vizuri, yasiyotibiwa na yanayopatiwa ufadhili kidogo kwenye utafiti.

Ni muhimu kushughulikia tofauti hii na kupanua wigo wa afya ya wanawake ili kujumuisha masuala haya muhimu. **BBC**



## Vijana BBT watakiwa kuchangamkia fursa uzalishaji mbegu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIJANA waliohitimu Programu ya Jenga Kesho Iliobora (BBT) chini ya Wizara ya Kilimo, wametakiwa kuchangamkia fursa ya uzalishaji mbegu bora iliyotolewa na Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA), ili kuongeza idadi ya wazalishaji mbegu hapa nchini.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa ASA, Dk. Sofia Kashenge, alisema vijana hao wana fursa kubwa ya kujikita kwenye uzalishaji mbegu kwa kuwa kuna soko.

"Tunawakaribisha pia vijana wa BBT kuomba fursa ya uwekezaji katika uzalishaji mbegu kwa sababu wanauelewa kuhusu kilimo na tulishawafundisha wakati wakiwa kwenye mafunzo,"alisema Dk Kashenge.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanashirikiana na wadau mbalimbali hapa nchini ili kuzalisha mbegu bora nchini.

"Tumejiwekea mikakati kuwa ili kufikia azma ya Rais Samia Suluhu Hassan katika suala la uwepo wa mbegu za kutosha ifikapo mwaka 2025 ni kuhakikisha wanatafuta wawekezaji wazawa ambao wanawekeza katika suala la mbegu ili tushirikiane," alisema.

Hivyo, aliwahimiza vijana kushawishika kuingia kwenye kilimo kwa sababu ni sekta kubwa yenye fursa nyingi za uzalishaji.

Hivi karibuni Rais Samia alisema ifikapo mwaka 2025, Tanzania inatakiwa kuzalisha asilimia 75 ya mbegu bora ambazo zitakidhi mahitaji ya wakulima hapa nchini.

# Wataalamu TEHAMA kujadili matumizi ya akili bandia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya TEHAMA (ICTC) inatarajia kufanya kongamano la kujadili, kuchochea mapinduzi ya teknolojia ya habari na mawasiliano nchini, ikiwamo matumizi ya akili bandia.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Nkundwe Mwasaga alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, kusema litakalofanyika kuanzia Oktoba 16 hadi 20, mwaka huu.

Alisema kongamano hilo litakutanisha wataalamu wa ndani na nje ya nchi ili kupata uzoefu wa teknolojia zinazotumika kwenye mataifa mengine ikiwamo akili bandia ili kutengeneza ajira kwa vijana na kuleta maendeleo ya kichumi na kijamii.

Dk. Mwasaga alisema hadi sasa kampuni 10 kutoka Misri, Estonia, Marekani na Ulaya zimethibitisha kushiriki katika kongamano hilo litakalolenga kubadilishana uzoefu kwenye TEHAMA na wataalamu wa hapa nchini.

Alibainisha kuwa ICTC imejipanga kuhakikisha wataalamu wa TEHAMA wanajengewa uwezo ili kutengeneza teknolojia ya akili bandia itakayokuwa ikitumia lugha ya Kiswahili.

Kadhalika, alisema kutokana na TEHAMA kuwa ni eneo jumuishi, wamedhamiria iguse makundi yote ikiwamo wanawake na vijana.

Hivyo, alitoa wito kwa wataalamu wa TEHAMA kuhudhuria ili kupata vitu vitakavyowaongezea ufanisi kwenye sekta hiyo ambapo wanapaswa kujisajili kupitia tovuti ya tume hiyo.

Akizungumzia kuhusu kongamano la sita la mwaka 20222, Dk. Mwasaga alisema walizungumzia kuhusu mapinduzi ya kidijitali na kati ya mambo yaliyozungumzwa ni gharama ya kusambaza huduma za intaneti kwa wananchi.

"Kulikuwa na gharama iliyokuwa ikitozwa ambayo ni Dola za Marekani 1,000 kwa kilomita na kwa kiasi kikubwa ilikuwa inatuletea changamoto kufikisha idadi ya watu ambayo Rais Samia Suluhu Hassan alisema ifikapo mwaka 2025 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia intaneti, kwa hiyo ile gharama ilikuwa inafanya gharama kwa watu wa mwisho ziwe kubwa," alisema na kuongeza:

Kadhalika, alisema kwenye kongamano hilo walizungumzia kuhusu suala la akili bandia kwa kuanza kuwajengea wataalamu uwezo na matumizi yaongezeke.

Pia alisema Tanzania inapaswa kupiga hatua kwa kiasi kikubwa kwenye eneo la akili bandia ili vijana wapate kazi na nchi ipate maendeleo makubwa ya kiuchumi.



Ofisa Maendeleo ya Jamii, Kata ya Kitunda, jijini Dar es Salaam, Rozina Soka, akichangia hoja kwenye kikao cha kujadili changamoto mbalimbali za kata hiyo kilichoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## SIFACU yaingilia tuhuma ubadhirifu fedha za wakulima

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Singida (SIFACU), kimevizuia vyama vya msingi (AMCOS) nane kujihusisha na ununuzi wa pamba katika msimu wa kilimo wa mwaka huu kutokana na viongozi wake kutuhumiwa kufanya ubadhirifu wa zaidi ya Sh.milioni 50.

Viongozi hao wanatuhumiwa kula pesa zilizotolewa na kiwanda cha kuchambua pamba kiitwacho Biosustain (T) Limited.

Mwenyekiti wa SIFACU, Yahaya Hamis alitoa kauli hiyo jana kuhusu hatua zilizochukuliwa na chama hicho baada ya mwekezaji wa kiwanda hicho kuvilalamikia baadhi ya vyama vya msingi katika mikoa ya Singida, Shinyanga na Simiyu kufuja fedha zilizotolewa kwa ajili ya kununua pamba kutoka kwa wakulima.

Hamis alisema Mkoa wa Singida una vyama vya msingi 52 ambapo kati ya hivyo 35 vinajishughulisha na ununuzi wa pamba lakini katika msimu wa 2022/23 vyama nane vilibainika kufuja fedha hizo zilizotolewa na kiwanda hicho.

Alisema fedha hizo zilifujwa kutokana na utaratibu mbovu unaotumiwa na wanunuzi kwa kupeleka fedha taslimu mkononi kwa makatibu wa vyama vya msingi kwa ajili ya kununua pamba kutoka kwa wakulima, hivyo baadhi ya viongozi wasio waaminifu wamekuwa wakizifuja fedha hizo.

Hamis alisema walishatoa mapendekezo kwa serikali kwamba fedha za ununuzi wa pamba ziwe zinawekwa kwenye akaunti za vyama vya msingi, lakini kutokana na ushindani wa ununuzi wa zao hilo jambo hilo halifanyiki kutokana na wakulima kutaka wapewe fedha taslimu mkononi waweze kununua mahitaji yao kwasababu wengine wanaishi mbali ambako hakuna huduma za benki.

Naye Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji mkoani Singida, Beatus Choaji, alisema serikali itahakikisha fedha hizo zinarejeshwa ili kutomkatisha tamaa mnunuzi huyo ambaye amekuwa mkombozi kwa wakulima wa pamba.

Choaji alisema katika msimu wa kilimo mwaka huu hadi kufikia Agosti 30 kilo 2,600 za pamba zimekusanywa kutoka kwa wakulima wa mkoani hapa na zimenunuliwa na mwekezaji wa kiwanda hicho.

## Serikali yazidi kujipanga kuelekea bima ya afya kwa wote

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeandaa mikakati ikiwamo kujenga vituo vya afya, kuajiri watumishi ikiwa ni maandalizi ya kuwezesha utekelezaji wa sera ya bima ya afya kwa wote.

Mratibu wa Fedha za Afya, Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe TAMISEMI, Dk. Dastan Mshana, alieleza hayo jana wakati wa maandalizi ya Kongamano la 10 la Afya Tanzania (THS) linalotarajia kufanyika Oktoba 3 hadi 5, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo litawaleta pamoja wadau zaidi ya 1,000 kujadili mfumo wa afya, upatikanaji wa huduma za afya kwa wote na huduma za afya ya msingi.

Dk.Mshana alisema kwa miaka mitano serikali imejenga vituo vya afya zaidi ya 1,800 pamoja na kuajiri watumishi wa afya zaidi ya 16,000.

Rais wa THS, Dk. Omary Chilo, alisema upatikanaji wa Huduma za Afya ya Msingi (PHC), uhitaji wa kuimarisha mfumo wa afya na mikakati ya kufikia Mpango wa Afya kwa Wote (UHC) ni masuala makuu yanayotarajiwa kupewa uzito wakati wa maadhimisho ya miaka 10 ya kongamano.

Alisema kongamano hilo litazikutanisha taasisi 50 ambazo zimethibitisha ushiriki wao, wawekezaji katika huduma za afya, wabunifu, wataalamu, viongozi wa serikali na viongozi wa sekta binafsi ili kujadili mwenendo na maendeleo ya huduma za afya nchini.

Dk. Chilo alisema kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Kuimarisha mifumo ya afya kwa ajili ya huduma za afya kwa wote'

Mwakilishi kutoka Baraza la Kiislamu Tanzania (BAKWATA), Dk.Zuhura Majapa, alisema katika kuhakikisha huduma bora za afya zinawafikia Watanzania wengi wamejenga vituo vya afya 33.

Alisema pia kuna washirika ambao wanashirikiana nao katika kutekeleza miradi mbalimbali ya afya.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Programu kutoka Kituo cha Kuzuia Magonjwa, Marekani (CDC), Dk. George Mgommela alisema wapo katika mazungumzo na serikali ya Tanzania kuhakisha wagonjwa wa HIV wanapata huduma za matibabu za magonjwa yasiyoambukiza.



# TPA yaipiga 'tafu' zahanati ya Ndadaro

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imetoa vitanda vitano vya kujifungulia na mashuka 200 katika Zahanati ya Ndadaro wilayani Kyela ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya Bandari nchini.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Manga Gasaya, alikabidhi msaada huo juzi huku watumishi wa Bandari za Ziwa Nyasa wakijitokeza kufanya usafi wa mazingira kwenye zahanati hiyo kama sehemu ya maadhimisho hayo.

Akikabidhi msaada huo, Gasaya alisema kuwa TPA imeamua kutoa msaada huo kama sehemu ya kuhudumia jamii inayowazunguka pamoja na kurejesha sehemu ya faida wanayoipata kwa wananchi.

"Msaada huu wa vitanda vitano vya kujifungulia na mashuka 200 vyote vina thamani ya shilingi milioni 10, sisi kama Mamlaka ya Bandari tumeamua kutoa msaada huu kwa lengo la kurejesha faida tunayoipata kwa wananchi lakini pia kuhudumia jamii yetu inayotuzunguka," alisema Gasaya.

Alisema kuwa uamuzi huo pia unalenga kuunga mkono jitihada za wananchi wa Kata ya Ndadaro walioamua kujenga zahanati hiyo kwa kutumia nguvu zao kabla ya kusaidiwa na serikali.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Swaum Kumbisaga, alisema msaada huo utaisaidia zahanati hiyo mpya kuanza kazi mara moja ili kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kyela.

Alisema kuwa zahanati hiyo imejengwa kimkakati ili kupunguza mlundikano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya ambayo kwa sasa imeelemewa.

"Hospitali ya Wilaya ya Kyela kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na msongamano wa wagonjwa kutokana na kwamba haikuwa na kituo kingine cha afya jirani, ndio maana Serikali kwa kushirikiana na wananchi tukajenga zahanati hii ya Ndandaro ambayo tunakusudia itoe huduma zote muhimu kwa wananchi ili kupunguza msongamano kwenye hospitali yetu ya wilaya," alisema Dk. Kumbisaga.

Alisema zahanati hiyo imekamilika, kujengwa hivi karibuni na kuzinduliwa na Mwenge wa Uhuru wiki iliyopita hivyo inao uhitaji mkubwa wa vifaa tiba ili ianze kutoa huduma zilizokusudiwa.

Kumbisaga aliwaomba wadau kutokeza kusaidia upatikanaji wa vifaa tiba ambavyo vinahitajika kwa lengo la kuwezesha zahanati hiyo kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Ndandaro walisema kukamilika kwa zahanati hiyo kutawasaidia kuondokana na kero ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu kwenye Hosptali ya Wilaya.

Sekela Nkanda, ambaye ni mkazi wa Kata ya Ndandaro alisema kuwa zahanati hiyo itakuwa yenye manufaa makubwa kwao kwa vile itawasogezea huduma za matibabu jirani na makazi yao.

"Tumefurahi kuona zahanati hii ikijengwa jirani, itatusaidia kupata matibabu jirani na hivyo kutumia muda wetu mwingi ambao tulikuwa tunaupoteza kwa kusafiri na kwenda hospitali ya wilaya kufanya shughuli zetu za kiuchumi," alisema Nkanda.

Ujenzi wa Zahanati ya Ndandaro umekamilika hivi karibuni na kabla haijaanza kutoa huduma kwa wananchi ilizinduliwa na Mwenge wa Uhuru wiki iliyopita.



Baadhi ya walimu wenye ulemavu wa aina mbalimbali mkoani Mbeya, wakiwa kwenye kikao na viongozi wa Chama cha Walimu nchini (CWT), mwishoni mwa wiki kilichokuwa na lengo la kujadili kero mbalimbali zinazowakabili kundi hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chanzo sekta ya usafirishaji kudidimia chatajwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

IMEELEZWA kuwa moja kati ya matatizo yanayokwamisha sekta ya usafirishaji nchini ni kusimamiwa na wizara zaidi ya tano ambazo kila moja ina tozo na sheria zake kitendo ambacho kinasababisha kuwepo na idadi ndogo ya wawekezaji wapya.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya mabasi ya ABC, Severine Ngallo, wakati wa uzinduzi wa ofisi za ABC Mkoa wa Njombe iliyogharimu zaidi ya Sh.milioni 100.

"Katika sekta hii tunafanya kazi na wizara tano, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Habari na Mawasiliano, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani ambazo kila wizara ina sheria zake na faini mbalimbali ambazo wawekezaji wengi wanashindwa kutekeleza ipasavyo jambo linalosababisha kuifanya kuwa biashara ya kurithishana, hivyo tunaomba uingalie kwa jicho la huruma" alisema Ngallo.

Ngallo alisema kampuni hiyo imekuwa ikitoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa zaidi ya miaka 30 na kisha kuwatoa hofu wakazi wa Njombe juu ya ubora wa huduma zinazokwenda kutolewa katika ofisi hizo. Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kassongwa, alisema uwekezaji huo unakwenda kuongeza mapato kwa halmashauri pamoja fursa ya ajira kwa vijana.

Alisema kuwa ujio wa wawekezaji wilayani humo umetokana na mazingira rafiki pamoja na hamasa ya muda ya mrefu kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika kilimo hususani parachichi na kisha kuendelea kualika wawekezaji wengine wa ndani na nje kuja wilayani humo kwa kuwa kuna utajiri wa ardhi yenye rutuba.

"Nitoe wito kwa wawekezaji wengine kuja Njombe kuwekeza na milango iko wazi na kwasababu biashara ya usafirishaji ni huria"alisema Kassongwa.

Alibainisha kuwa: "Rais Samia Suluhu Hassan, aliagiza sisi wawakilishi wake kubuni vyanzo vingi vya mapato na ujio wa mradi huu wa ofisi ya ABC ni kimoja wapo, hivyo tunaendelea kukaribisha wawekezaji wengine wa ndani na nje ya Njombe kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali kwa kuwa Njombe ina ardhi ya kutosha kwa wawekezaji,ofisi hii ni ya kisasa"alisema.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, Masoud Kwileka, alisema ujio wa ofisi hiyo utasaidia kudhibiti vishoka wanaokatisha tiketi na kuwaibia abiria.

Pia alitumia fursa hiyo kusisitiza kuzingatia sheria za barabarani kwa ajili ya usalama wa abiria na mizigo yao.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Merickzedeck Kaberege, alisema halmashauri ilitoa fursa ya mwekezaji huyo kwasababu anakwenda kuchochea ukuaji wa fursa nyingine za uchumi na kisha kuwataka wawekezaji wengine kuja kuwekeza.

## Serikali yatoa maagizo kwa wazalishaji vifaa vya ujenzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewataka wazalishaji wa vifaa vya ujenzi kuzingatia ubora, ili kuwasaidia wananchi na serikali kutotumia gharama kubwa kuifanyia ukarabati miradi inayojengwa kwa kutumia vifaa visivyo na ubora.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara kwenye baadhi ya viwanda vinavyozalisha mabati jijini Mbeya.

Homera alisema ili maendeleo yapatikane kwa haraka ni muhimu serikali ishirikiane na wadau wa sekta binafsi kwa kuwa pande hizo mbili zinategemeana katika kufanikisha malengo yao.

"Nawapongeza sana wawekezaji wa viwanda hivi vya kuzalisha mabati hapa mkoani kwetu mnachokifanya ni sehemu ya kuiunga mkono serikali kwenye utekelezaji wa miradi ili tujenge vyumba vya madarasa na vituo vya afya lazima tutumie mabati," alisema Homera.

Aliongeza kuwa mkoa huo una maeneo mengi yenye fursa za kibiashara na ongezeko la idadi ya watu hali inayochochea maendeleo ya kiuchumi, hivyo akawataka wadau wa maendeleo kuwekeza biashara zao kwenye mkoa huo ili kukuza uchumi wao.

Meneja Matawi wa Kampuni ya ALAF, Naeem Abdul, alisema kampuni hiyo imefanya kazi kwa miaka zaidi ya 60 nchini kwa kuendelea kuboresha huduma zao na kufungua matawi kwenye mikoa mbalimbali Nchini.



# ‘Serikali kinara uimarishaji demokrasia, siasa Afrika’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania, Juma Ali Khatib, amesema Tanzania imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuimarisha suala la demokrasia na siasa ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika.

Aliyasema hayo jana wakati alipokutana na uongozi wa Taasisi ya Mpango wa Hiyari wa Nchi za Umoja wa Afrika Kujipima katika vigezo vya Utawala Bora (APRM Tanzania), katika Ofisi za Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar.

Alisema katika uso wa dunia Tanzania ina taswira nzuri na kubwa kuhusu masuala ya utawala bora kutokana na usimamizi mahiri wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha ukomavu katika siasa na kufungua milango ya demokrasia.

Juma ambae pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Ada Tadea, alisema kitendo cha Rais Samia kuruhusu mikutano ya hadhara na kutoa nafasi katika ushirikishwaji wa wananchi ni kitendo cha kupongezwa kawa sababu kimefungua milango ya demokrasia na utawala bora.

Naye Katibu Mtendaji wa APRM Tanzania, Lamau Mpolo, alisema vyama vya siasa ni wadau muhimu kwa taasisi yao, hivyo watahakikisha maoni na michango yao inachukuliwa katika uandishi wa ripoti ya pili ya tathmini ya masuala ya utawala bora Tanzania.

Aidha, alisema katika kutekeleza majukumu yao taasisi yao imedhamiria kufanya tathmini ya pili ya utawala bora nchini licha ya ile ya kwanza iliyofanywa mwaka 2013.

Lamau alisema taarifa za APRM zina umuhimu mkubwa katika masuala ya utawala bora na inawahusu wananchi hasa kutimiza dhana inayoungwa mkono duniani kuhusu utawala shirikishi unaowapa wananchi fursa ya kuishauri serikali.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa taasisi hiyo, Badria Attai Masoud, aliahidi kwamba APRM itahakikisha inamfikia kila mwananchi mjini na vijijini ili kutoa maoni yao kuhusu utawala bora Tanzania na kuingizwa katika ripoti hiyo ya pili.

APRM inafanya tathmini ya pili katika mambo matano ikiwemo siasa na demokrasia, ukuaji wa uchumi, utoaji wa huduma jamii kwa wananchi ikiwemo maji, umeme, afya na huduma nyingine.

Pia wanafanya tathmini katika usimamizi wa kampuni binafsi kuona endapo wana sera rafiki ambazo zinatoa ajira kwa wananchi, mapato, kuzingatia haki za wafanyakazi na utayari wa nchi kupambana na majanga na misukosuko ikiwemo ugonjwa wa virusi vya corona, vita na majanga mengine.

# Serikali yalipa mil.58/- kupeleka umeme Soko la Samaki Tumbe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesema imetumia Sh. milioni 58.7 kulipa fidia wananchi walioathiriwa mazao, mali wakati ikipeleka umeme katika Soko la Samaki Tumbe.

Waziri wa wizara hiyo, Masoud Suleiman Makame alibainisha hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Omar Fakihi aliyetaka kujua fidia iliyotumika kutokana na umeme huo.

Akijibu swali hilo, Makame alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imeipatia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi jumla ya shilingi milioni 58.7 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi walioathiriwa wakati wanapitisha umeme huo kuelekea katika soko hilo.

Aidha, alisema wananchi 39 kati ya 40 ikiwemo taasisi moja ya serikali wameshafanyiwa malipo yao yenye thamani ya Sh. milioni 58.5 sawa na asilimia 99.6 ya malipo yote.

Waziri huyo alisema bado Wizara haijapata vielelezo vyovyote vinavyomuhusu mtu mmoja aliyebakia na ambae bado hajalipwa Sh. 210,000.

“Mheshimiwa Spika, Kufuatia majibu A na B Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inathibitisha kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tayari imechukua hatua zinazostahiki katika kufanya malipo kwa wananchi walioruhusu suala la maendeleo la kupelekewa umeme katika Soko la Tumbe” alisema.




Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania Limited, Benoit Araman, akizungumza kwenye mkutano wa waandishi wa habari mjini Unguja Zanzibar mwishoni mwa wiki, alipotangaza kuungana kwa kampuni za gesi ya Oryx Gas Zanzibar Limited na TP Company Limited ya Zanzibar ambayo ni kampuni tanzu ya Vigor Turky’s Group of Companies ili kuwezesha wakazi wa Zanzibar kupata nishati safi ya LPG kwa gharama nafuu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matengenezo Mv Mapinduzi yafikia asilimia 70

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema ameridhishwa na hatua za matengenezo ya Mv Mapinduzi namba mbili ambayo imesitisha safari zake za kutoka Unguja kwenda Pemba.

Meli hiyo ambayo kwa sasa imepiga nanga katika Bandari ya Malindi visiwani hapa inaendelea kufanyiwa matengenezo baada ya kuharibika.

Akizungumza wakati alipofanya ziara ya kukagua matengenezo ya meli hiyo, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuifanyia matengenezo meli hiyo ili kuwasaidia wananchi hasa wa Pemba na Tanga kupata usafiri salama na wa uhakika.

Alisema amefurahishwa na matengenezo ya meli hiyo, kwamba yanaendelea vizuri na yameshafikia kwa asilimia 70, inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi michache ijayo.

Aidha, alisema kukamilika kwa matengenezo ya meli hiyo kutaondoa tatizo la usafiri linalowakabili wananchi husani wakazi wa Kisiwa cha Pemba ambao hutegemea usafiri wa meli kwa shughuli zao.

Hemed aliwataka wahandisi na wataalamu elekezi kusimamia kwa umakini matengenezo ya meli hiyo, kuheshimu makabaliano ya mkataba ili kuhakikisha wanafanya kazi nzuri na kwa ubora unaotakiwa.

Alisema serikali inatumia gharama kubwa katika kuifanyia matengenezo meli hiyo, hivyo ni wajibu kwa makandarasi kuhakikisha wanatumia vifaa vilivyo bora na vitakavyodumu kwa muda refu.

Kadhalika, alisema serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu na umakini kuhakikisha meli hiyo inakamilika kwa wakati uliopangwa na kuahidi endapo kutatokea changamoto yoyote katika matengnezo hatua za haraka zitachukuliwa.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhamed, alisema kuwa wizara kupitia Shirika la Meli Zanzibar inafuatilia kwa karibu matengenezo hayo ili meli hiyo ikamilike Desemba mwaka huu na kwa ubora uliokusudiwa.

Alisema katika kipindi hiki cha matengenezo ya meli hiyo Wizara ilipata changamoto ya vifaa kutoka Ujerumani iliyosababisha kuvisafirisha kupitia Korea kufika Zanzibar, hatua ambayo imesababisha kuchelewa kufanya kazi kwa muda wa miezi miwili.

Mkurugenzi wa Shirika la Meli Zanzibar, Makame Hasnuu Makame, alisema kuwa hadi sasa matengenezo hayo yamefikia asilimia 70, kwamba hatua inayoendelea sasa ni kufunga mashine na meli hiyo inategemewa kukamilika ifikapo Oktoba mwaka huu.

Alisema shirika litaendelea kusimamia matengenezo hayo ili kuhakikisha meli hiyo inakamilika kwa wakati na itumike kwa kutatua changamoto ya usafiri kwa wananchi wanaosafiri kati ya Unguja, Pemba na Tanga.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**THERESIA ROBERT NUMVIRE**

MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA CHETI CHA FORM FOUR ( CSEE ) CHENYE INDEX **NO: S 2325-0064** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA SHULE YA SEKONDARI CANOSSA MWAKA 2012. TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA KINONDONI NA KUPEWA RB NO: **PHQ/DAR/KIN/13821/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......52/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MOHAMED BURHAN MWENGO wa KIHONDA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RASHIDI MOHAMED MWENGO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 09 mwaka 2023

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 79 OF 202**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE OF THE LATE JACOB MATONYA MWIMBWA of Iyumbu within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY GILBERT MATONYA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 09, 2023.

Dated at Dodoma this 16 day of 08, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI ARUSHA**

**SHAURI LA MAOMBI LA MADAI NA. 316/02 YA 2017**

**HELLEN DANIEL LAUWO NA MWENZAKE.....................................MLETA MRUFANI**

**DHIDI YA**

**STANDARD CHARTERED BANKLTD NA WENZAKE...........................................MJIBU RUFANI**

**KWA:**
**HELLEN DANIEL LAUWO**

**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na mahakama hii Arusha tarehe 25 Septemba, 2023 saa tatu (03:00) kamili asubuhi. Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 06 septemba, 2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU (T)
ARUSHA

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 426 LA 2014**

**SAGO WILDEN SAGO...........MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**RID MAJOR JOHN J. MKONO...MDAIWA/WADAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**RID MAJOR JOHN J. MKONO – POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SAGO WILDEN SAGO** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 12/10/2023 saa 3:00am Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 18 Mwezi wa 09/2023.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RUTI JOHNSON MWAMFUPE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenye usajili namba **T 949 AYH ,** CHASSIS NAMBA: **TD01W217651** na ENGINE NAMBA: **G16A406958.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/2531/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YAKOBU MICHAEL LUGENDO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CARINA** yenye usajili namba T 112 CGL , CHASSIS NAMBA: AT2120063240 na ENGINE NAMBA: 5AH364373. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/2532/2023**

---

**FOMU MADAI - 3**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 1028/2023**

**Jina la VERONICA BERNARD MNDOLWA............MDAI**

**Jina la CONRAD DOHA KAGAMBO.............MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa CONRAD DOHA KAGAMBO**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao**
**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 10 Mwezi wa 8 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi mbele ya Mhe. MWAGENI kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vilelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **6 Mwezi wa 7 Mwaka 2023.**

---

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI [ SURA 334 ]**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI**

**MUOMBAJI: GETRUDE MSEMWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA WILLIAM MWAKAGALI**
**S.L.P 190, MAFINGA**

**MMILIKI ALIEANDIKISHWA WILLIAM MWAKAGALI**
**S.L.P 141, MUFINDI.**

**ARDHI: KIWANJA NAMBA 37 KITALU 'A' JOHN'S CORNER URBAN AREA.**

**HATI NAMBA: 21194.**
**TAARIFA IMETOLEWA; KWAMBA HATI YA KUMILIKI ARDHI ILIYOTAJWA APO JUU**

IMEPOTEA NA NNAKUSUDIA KUTOA HATI MPYA BADALA YAKE IWAPO HAKUNA
PINGAMIZI KWA MDA WA MWEZI MMOJA TOKEA TAREHE YA TAARIFA HII ITAPO
TANGAZWA KATIKA GAZETI LA SERIKALI.
HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa msajili wa Hati msaidizi 785 IRINGA
S.L.P 785, IRINGA.

Imesainiwa leo tarehe 22 mwezi june 2023.

J.G.Mwenda
MSAJILI WA HATI MSAIDIZI
MKOA WA IRINGA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration cause No. 97 ...OF 2023**

**In the matter of the estate of the late NG'AMBI MZANJE MATEBE**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by EMMANUELI MPALI MASING'OTI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 day of ....10....2023
**Dated at Dodoma this 13 day of ....09.... 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**WORLD VISION TANZANIA** anatangaza kupotea kwa kadi nne za pikipiki aina ya **HONDA XL 125** zenye namba za usajili **MC 360 CZP,** Chassis No. **LTMJD2192F5335987, MC 361 CZP,** Chassis No. **LTMJD2190F5336023. MC 362 CZP,** Chassis No. **LTMJD2198F5336013** na **MC 363 CZP,** Chassis No. **LTMJD2197F5336004.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/DOD/DOD/858/2023.**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 00745 700 710.***




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA/ KITAIFA

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Wakili: Dada wa kazi alisaidia wahalifu

Na Grace Gurisha

ALIYEKUWA dada wa kazi wa Aneth Msuya, Getruda Mfuru, amedai hajashiriki kusaidia wahalifu kufanya uhalifu licha ya kwamba aliondoka nyumbani siku moja kabla ya tukio la mauaji ya bosi wake.

Getruda alidai hayo mwishoni mwa wiki iliyopita mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akiulizwa maswali ya dodoso na Wakili wa Utetezi, Nehemiah Nkoko katika kesi hiyo ya mauaji inayowakabili Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela.

Wakili Nkoko alimwuliza Getruda maswali mbalimbali kutokana na tukio la mauaji ya Aneth kwa kuwa yeye ndiye alikuwa mtu wa karibu wa marehemu.

**Nkoko:** Nitakuwa sahihi kwa wakati ule kuwa mtu pekee Aneth aliyekuwa anamwamini kubaki na mali zake zote ni wewe?

**Shahidi:** Ni kweli

**Nkoko:** Na hata kwa maisha yake, kwa sababu wewe ndiwe ulikuwa unapika chakula?

**Shahidi:** Ni kweli, mimi nilikuwa ninapika.

**Nkoko:** Na nitakuwa sahihi kwamba ulikuwa unaaminiwa kufanya usafi wa nyumba nzima na nje?

**Shahidi:** Ndiyo, ni mimi nilikuwa ninafanya usafi wa mazingira ya ndani na nje.

**Nkoko:** Wewe ndiwe ulikuwa unakwenda kununua mahitaji ya ndani?

**Shahidi:** Hapana, dada alikuwa ananunua vitu mwenyewe, anatoka navyo mjini.

**Nkoko:** Kama ni hivyo, nini kilikufanya ukanunue 'toilet paper' dukani? Nini kilikusukuma?

**Shahidi:** Alipokuwa anaondoka, aliniambia nikanunue.

**Nkoko:** Ni siku zipi Aneth alikuwa anashinda nyumbani?

**Shahidi:** Ni Jumapili chache alikuwa anashinda nyumbani, si zote, zingine anakwenda kazini.

**Nkoko:** Kwahiyo na siku za Jumapili anakwenda kazini?

**Shahidi:** Yeye alikuwa anaaniaga kwamba anakwenda kazini. Sasa siwezi kujua kuwa yeye anakwenda kazini au la.

**Nkoko:** Nitakuwa sahihi kwamba wewe ndiwe uliyetoa taarifa za ndani za bosi wako kuwasaidia wahalifu kufanya uhalifu wao?

**Shahidi:** Mimi sikuhusika kuwasaidia wafanye uhalifu huo.

**Nkoko:** Mbona wewe uliondoka nyumbani tarehe 25/5/2016, siku moja kabla ya tukio?

**Shahidi:** Mimi sikuhusika.

**Nkoko:** Kama mahakama ingeamini hawa washtakiwa ndiyo wameua na wewe uliahidiwa Sh. milioni 50, ukapewa simu, 20,000/- na wewe si mhusika kabisa?

**Shahidi:** Mimi sio mhusika wa hicho kitendo. Nilipewa kwa kutishwa.

**Nkoko:** Lakini ulipokea!

**Shahidi:** Ndiyo, kwa vitisho vikali.

**Nkoko:** Wewe ulikaidi kurudi nyumbani baada ya ujumbe uliotumiwa na Aneth kwamba urudi nyumbani uondoke kwa usalama?

**Shahidi:** Mimi sikukaidi ila vitisho ndivyo vilivyosababisha.

**Nkoko:** Nitakuwa sahihi baada ya wewe kutoroka, taarifa zikaja kwamba dada Aneth alichinjwa kinyama kama wewe ulivyosema?

**Shahidi:** Nilipata taarifa tarehe 26/5/2016 na tarehe 25/5/2016 ndiyo niliondoka.

**Nkoko:** Utakubaliana na mimi kwamba hakuna mtu yeyote wa Dar es Salaam aliyekwambia taarifa za msiba wa Aneth?

**Shahidi:** Kwa kweli sikumbuki.

**Nkoko:** Hukumbuki kama ulipewa taarifa?

**Shahidi:** Kwa kweli sikumbuki.

**Nkoko:** Mtu wa mwisho kutoka nyumbani kwa Aneth Msuya ni Getruda Mfuru?

**Shahidi:** Kwa kweli siwezi kujua nani mwingine aliingia huko nyuma, dada alivyokuja na kutoka sijui nani mwingine aliingia.

**Nkoko:** Wakati wewe unaondoka saa tano na nusu asubuhi mtoto alikuwa wapi?

**Shahidi:** Alikuwa shuleni.

**Nkoko:** Utakubaliana na mimi kwamba mtoto alikuwa anasoma 'nursery' na 'nursery' wanatoka saa sita mchana?

**Shahidi:** Ndiyo, alikuwa anasoma nursery na ni kweli anatoka saa sita mchana. Siku hiyo mama yake aliniambia atamfuata mwenyewe shuleni.

**Nkoko:** Utakubaliana na mimi kwamba siku ya tarehe 25/5/2016 ilikuwa Jumatano. Sasa mtoto anapelekwa kuogolea?

**Shahidi:** Sikumbuki siku, lakini mimi ninakumbuka ilikuwa tarehe 25/5/2016.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake huyo, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

Aneth, dada wa marehemu Erasto Msuya, maarufu Bilionea Msuya, aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam.

UHABA WA MAJI;

## Waafrika Kusini watakiwa kuoga chini ya dakika mbili

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

WASAMBAZAJI wa maji mjini Johannesburg, Afrika Kusini, wamewataka wakazi wa jiji hilo na vitongoji vyake kutumia maji kidogo huku uhaba wa maji ukitishia kuanguka kwa mfumo.

Rand Water na Johannesburg Water, mwishoni mwa wiki zilisema matumizi makubwa ya maji kwa wakazi yanatatiza mfumo na imesababisha viwango vya chini vya hifadhi ya maji.

Kampuni hizo zimewataka wakazi kuokoa maji kwa kupunguza kuoga hadi dakika mbili tu, kutumia chooni baada ya haja kubwa na kuosha magari wikiendi pekee kwa kutumia ndoo.

Kampuni hizo pia, zimewataka wakazi kuacha kujaza maji katika vidimbwi vya kuogelea hadi uhaba wa maji uishe, kutomwagilia bustani na nyasi kwa kutumia maji safi na kurekebisha au kutoa taarifa kuhusu uvujaji wa maji.

Johannesburg, kwa sasa iko chini ya vikwazo vya kila mwaka vya maji, ambavyo mara nyingi hudumu wakati wa kiangazi kati ya Septemba na Machi.

Katika wiki za hivi karibuni, baadhi ya wakazi wa jiji hilo na taasisi kama vile hospitali, zimekosa maji na kusababisha taharuki kwa umma. **BBC**



Rais Denis Nguesso. **PICHA: MTANDAO**

## Congo 'yanusa' jaribio la mapinduzi

**Brazzaville,** CONGO

SERIKALI ya Congo-Brazzaville, imetupilia mbali ripoti za kuwapo kwa jaribio la mapinduzi ya kijeshi dhidi ya utawala wa Rais Denis Nguesso, ambaye ametawala kwa kipindi cha miaka 39.

Kauli ya serikali inakuja baada ya taarifa kusambaa kwenye mitandao ya kijamii mwishoni mwa wiki, kwamba jeshi lilikuwa linajaribu kuangusha utawala wa kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 79 anayehudhuria mkutano wa awamu ya 78 wa Umoja wa Mataifa (UN), jijini New York.

Ujumbe kwenye ukurasa wa X zamani ukijulikana kama twitter, Waziri wa Mawasiliano kwenye taifa hilo Thierry Moungalla, alisema taarifa hizo ni za uongo.

Waziri huyo aliwahakikishia raia wa Congo kuwa nchi yao iko salama na hakuna hofu yoyote na waendelee na shughuli zao za kila siku.

Wito kama huo pia ulichapishwa kwenye tovuti ya serikali, ukitaja ripoti hizo za mapinduzi kama zisizokuwa za kweli. Rais Nguesso, aliingia madarakani katika taifa hilo lenye utajiri wa mafuta kupitia mapinduzi ya kijeshi mwaka wa 1979.

Alishindwa katika uchaguzi wa vyama vingi mwaka wa 1992 kabla ya kurejea uongozini tena mwaka wa 1997, baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kiongozi huyo wa Congo, ndiye rais wa tatu ambaye amekuwa madarakani kwa muda mrefu zaidi barani Afrika, baada ya mwenzake wa Equatorial Guinea, Teodoro Obiang na wa Cameroon, Paul Biya.

Kumekuwa na wimbi la mapinduzi barani Afrika katika miezi ya hivi karibuni, hivi punde katika nchi jirani ya Gabon, ambako jeshi lilinyakua mamlaka Januari, mwaka huu. **RFI**

HABARI MICHEZO

# KOPUNOVIC AONA MABADILIKO TABORA UTD AKIIWINDA COASTAL

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Tabora United, Goran Kopunovic, amesema timu yake imeanza kupata muunganiko licha ya kwamba bado anahitaji muda wa kuendelea kuifanya kuwa tishio kwenye Ligi Kuu Bara.

**Tabora United juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Tanzania Prisons, katika mchezo wa ligi hiyo uliopigwa katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mjini Tabora.**

Akizungumza na Nipashe jana, Goran alisema hawakuwa na muda wa kufanya maandalizi ya msimu mpya pamoja, jambo lililomfanya kutumia mechi zao za mwanzo kama sehemu ya kujiandaa huku akitengeneza muunganiko wa timu yake na kusaka matokeo.

Alisema kwenye mechi tatu walizocheza za ligi, alipoteza dhidi ya Azam FC, Suluhu na Singida Fountain Gate FC na katika ushindi dhidi ya Tanzania Prisons, ameona mabadiliko huku akitarajia kupata muunganiko mzuri mbeleni.

"Hatukuanza vizuri ligi, tulipoteza, tukasuluhu na tumeshida mechi yetu ya tatu, inaonesha kuwa tumeanza kukaa vizuri, lakini bado tunaendelea kutumia mechi hizi kusaka pointi pia nikiendelea kutengeneza muunganiko kwa wachezaji wangu," alisema Kopunovic.

Aliongeza kuwa anaimani kikosi chake kitazidi kuimarika zaidi kwa kila mechi na kufanya vizuri kwa kufikia malengo wanayotarajia kwa msimu wao wa kwanza katika ligi hiyo.

Kuhusu mechi yao ijayo dhidi ya Coastal Union, kocha huyo alisema wanaendelea na maandalizi ili kutimiza malengo yao makubwa ya kuondoka na alama tatu kwa kila mechi iwe ugenini au nyumbani.

Tabora United watakuwa ugenini jijini Tanga dhidi ya Coastal Union katika mchezo utakaopigwa Septemba 29, mwaka huu, Uwanja wa Mkwakwani.



## 'MUUAJI'...



Straika wa Singida Fountain Gate na mfungaji wa bao pekee dhidi ya Future FC ya Misri, Mkenya Elvis Baranga Rupia, akiwania kumiliki mpira dhidi ya Wamisri hao kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Singida FG ilishinda bao 1-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Aiyee aibeba Mbuni Championship*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Mwadui FC, Salum Aiyee, juzi alipachika mabao mawili akiiongoza timu yake mpya ya Mbuni FC kuichakaza Stand United 3-1 katika mechi ya raundi ya pili Ligi ya Championship iliyochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Aiyee ambaye alishika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu msimu wa 2018/19 kwa kupachika mabao 18 akiitumikia Mwadui FC, akizidiwa na mshindi wa Kiatu cha Dhahabu msimu huo, Meddie Kagere, aliyekuwa akichezea Simba kwa mabao yake 23.

Juzi Aiyee alifunga mabao yake dakika ya 17 kutokana na makosa ya kipa wa Stand United Paul Kamtewe, kuuchezea mpira kwenye eneo la hatari, straika huyo akamnyang'anya na kuukwamisha wavuni.

Dakika nne baadaye aliweka lingine kutokana na makosa mengine ya kipa aliyetokea langoni kumfuata, mfungaji akaubetua na ukajaa wavuni.

Kabla ya Aiyee kupachika mabao hayo, tayari Mbuni ilikuwa imeshatangulia kufunga bao moja lililopachikwa nyavuni sekunde ya 50 na Emmanuel Mtumbuka 'Okwi', linakuwa bao la mapema zaidi mpaka sasa kwenye ligi hiyo.

Said Zanda, aliifungia Stand United bao la kufutia machozi dakika ya 69 akitokea benchi.

Matokeo ya mechi zingine zilizochezwa juzi, Fountain Gate Academy ilichapwa mabao 2-1 nyumbani na Mbeya Kwanza, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, huku Mbeya City ikirejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa kuishindilia Transit Camp mabao 2-0, Uwanja wa Sokoine Mbeya, yote yakiwekwa wavuni na Maulid Shaaban.

Mbeya City inaongoza ikiwa na pointi sita na mabao saba, ikifuatiwa na Pamba FC ambayo pia ina pointi sita, lakini ina mabao matano ya kufunga.



# Kampeni ya ZFF kuvutia mashabiki viwanjani yajibu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar ukikamilika timu nne tu kuvuna alama zote tatu, kampeni maalum ya hamasa ya kwa mashabiki kujitokeza uwanjani kwa wingi imeanza kuzaa matunda, imeelezwa.

Katika mechi za mzunguko huo wa kwanza, timu zilizofanikiwa kuvuna alama zote tatu ni Zimamoto ambayo iliifunga Ngome FC huku Mlandege ikiibuka kidedea dhidi ya Chipukizi kama ilivyo kwa KVZ iliyoichapa Maendeleo SC na timu ya JKU ikifanya hivyo dhidi ya New City.

Timu nane zimevuna alama moja baada ya kutoka sare katika michezo yao hiyo, ambazo ni KMKM ililazimishwa sare na Uhamiaji wakati Mafunzo hali ikiwa hivyo dhidi ya Hard Rock, Kipanga FC nayo ikitoka sare dhidi ya Malindi SC huku Kundemba FC ililazimishwa sare na Jamhuri.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Suleiman Salum, alisema ameridhishwa na mwamko wa mashabiki wa soka visiwani Zanzibar kujitokeza kwa wingi viwanjani katika mechi hizo za raundi ya kwanza kushuhudia timu zao.

Alisema katika mzunguko huu wa kwanza ulikuwa wenye mafanikio makubwa hasa katika lile lengo la kurejesha hamasa kwa mashabiki wa Zanzibar kwenda uwanjani kushuhudia mechi za Ligi Kuu.

Salum alisema ZFF kwa kushirikiana na wadau wa soka wataendelea na jitihada za kufanyia kazi changamoto mbalimbali zitakazojitokeza kwa kila mzunguko wa Ligi Kuu ili kuiboresha na kuwavutia watazamaji kuweza kuifuatilia ligi yao.

"Kwa mzunguko huu wa kwanza tumefanikiwa kuwaleta mashabiki uwanjani, na umekwenda kama tulivyotarajia, hivyo lazima tuzidishe juhudi kwa kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha tunafanikiwa na kuvuka hadi lengo," alisema.

Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa pili itaendelea leo Jumanne ambapo Maendeleo FC itashuka dimbani kuikabili Mlandege FC katika dimba la Finya, Unguja huku Kundemba FC ikiwakaribisha Mafunzo katika dimba la Mau A.

## ZISIKUPITE

### MCTOMINAY ATAKIWA BAYERN

KIUNGO wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay, 26, ameibuka kuwa chaguo la Bayern Munich iwapo watamkosa Joao Palhinha wa Ureno, 28, kutoka Fulham Januari. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAMZUIA JAMES

INGEKUWA ofa "ya kipuuzi" kwa Chelsea kufikiria kumuuza Reece James, 23, anayelengwa na Real Madrid kwa sababu beki huyo wa England yuko chini ya mkataba hadi 2028. ***(Football Insider)***

### WILLIAMS AWINDWA VILLA

KLABU ya Aston Villa imeungana na Liverpool na Barcelona katika mbio za kutafuta saini ya winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams, 21, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao. ***(Diario AS)***

### BARCO ATAJWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inatarajiwa kuwasilisha ofa mpya ya kumnunua beki wa Boca Juniors Valentin Barco, 19, kabla ya dirisha la uhamisho la Januari. ***(Sun)***

### MORATA ATEGWA ROMA

KLABU ya AS Roma inafikiria kuendelea na ombi la kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata, 30, kutoka Atletico Madrid baada ya kufanya mazungumzo na wakala wa mchezaji huyo. ***(Corriere dello Sport)***

### AWAKALIA NA WASAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Italia, Ciro Immobile, 33, anatarajiwa kusalia Lazio, licha ya kupokea ofa kutoka kwa klabu za Saudia. ***(Corriere dello Sport)***

### LOW ANUKIA UTURUKI

KOCHA wa zamani wa Ujerumani, Joachim Low ni miongoni mwa wagombea wanaopigiwa upatu kuchukua nafasi ya Mjerumani mwenzake, Stefan Kuntz kama kocha wa Uturuki. ***(DHA)***

### MONTELLA NAYE ATAKIWA

SHIRIKISHO la Soka nchini Uturuki limeanza mazungumzo na mshambuliaji wa zamani wa Italia, Vincenzo Montella, ambaye aliinoa Adana Demirspor ya Uturuki kwa miaka miwili, kuhusu kurithi nafasi ya Stefan Kuntz. ***(Nicolo Schira)***

### EKITIKE NA WEST HAM

KLABU West Ham na Crystal Palace huenda wakafufua nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Paris St-Germain, Hugo Ekitike, 21, katika dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### OSCAR KWA VIGOGO EPL

KLABU za Manchester United, Arsenal na Liverpool zinamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, 19, Oscar Gloukh, ambaye sasa anaichezea Israel mara kwa mara. ***(Sun)***

### GALLAGHER ANANYATIWA

MCHEZAJI Conor Gallagher, 23, anayenyatiwa na Tottenham Hotspur huenda akabadilisha msimamo wake kuhusu mustakabali wa klabu yake na kuamua kuondoka Chelsea ikiwa kiungo huyo wa England atapoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza mara baada ya kupona jeraha. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AANIKA SABABU YA KUBADILISHA MAKIPA WAKE

**LONDON,** England

**Hisia zangu ni kumfanya kila mtu ashiriki katika timu, bila kujali ushindani, lazima...**

MIKEL Arteta amefichua kuwa amefikiria kuwabadilisha makipa wake, Aaron Ramsdale na David Raya, katika michezo ya karibuni.

**Hali ya mlinda mlango wa Arsenal imekuwa gumzo miongoni mwa mashabiki tangu klabu hiyo ilipofanya uamuzi wa kumsajili David Raya aliyetua kwa mkopo kutoka Brentford wakati wa majira ya joto.**

Ramsdale alishikilia nafasi ya kuanza kwa mechi nne za kwanza za msimu wa Ligi Kuu ya England, hata hivyo Raya hatimaye alipangwa katika mchezo wa Arsenal na Everton Jumapili - mchezo ambao walishinda bao 1-0 pale Goodison Park.

Baada ya ushindi huo, Arteta aliulizwa na waandishi wa habari kuhusu uamuzi wa kumuanzisha Raya mbele ya Ramsdale.

"Mawazo yale yale ambayo Fabio Vieira alicheza hapa au Eddie Nketiah alicheza badala ya Gabriel Jesus. Sijawa na swali hata moja kwa nini Gabriel Jesus hajaanza. Ameshinda mataji mengi zaidi ya mtu yeyote, nikiwamo mimi.

"Ni kitu ambacho kimefanywa kihistoria kama hiki, lakini siwezi kuwa na wachezaji wawili kama hawa katika nafasi moja na nisiwacheze. David ana sifa nzuri kama vile Aaron anazo."

Arteta aliendelea kusema kwamba alifikiria kuwabadilisha makipa wake katika mechi za hivi karibuni akikiri kwamba "najuta" kwa kutofanya hivyo.

"Iko hivi. Mimi ni kocha mchanga sana. Nimekuwa kwenye kazi hii kwa miaka mitatu na nusu na sijutii kwa kile nilichokifanya.

"Mojawapo ni kwamba katika nyakati mbili, nilihisi dakika 60 na dakika 85, katika michezo miwili, katika kipindi hiki, kubadilisha kipa katika wakati huo. Lakini sikufanya hivyo. Sikuwa na ujasiri wa kufanya hivyo. "Lakini nina uwezo wa kuchukua winga au mshambuliaji, au beki wa kati juu ya kushuka hadi tano na kushikilia matokeo hayo.

"Tulitoka sare kwenye michezo hiyo na sikuwa na furaha. Hiyo ni ajabu? Kwa nini? Tuna sifa zote kwa kipa mwingine kufanya kitu wakati kitu kinatokea na unataka kubadilisha kasi.

"Sasa hisia zangu ni kumfanya kila mtu ashiriki katika timu. Wanapaswa kucheza, bila kujali ushindani. Lazima tufanye hivyo. Huu ni ujumbe wangu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,154,8

MECHI KALI
PARIS ST. GERMAIN
VERSUS
BORUSSIA DORTMUND
1 | 1.77
X | 3.74
2 | 3.88

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Tumaini Kileva - 0652 942 XXX
2. Hamza Ramadhani - 0653 407 XXX
3. Brighton Buberwa - 0654 567 XXX
4. Presiosa Kalage - 0659 922 XXX
5. Mussa Mwichande - 0659 096 XXX
6. Sauli Mwanitega - 0673 153 XXX
7. Clement Mayangula - 0674 955 XXX
8. Yumna Hababuu - 0678 149 XXX
9. Emanuel Wami - 0678 434 XX
10. Noro Noro - 0717 330 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POCHETTINO SASA ALALAMIKIA WACHEZAJI WAKE CHELSEA



**LONDON,** England

KOCHA Mauricio Pochettino, amelalamikia ugumu wa Chelsea mbele ya lango baada ya kutoka suluhu na Bournemouth Jumapili.

Katika mchezo wa pili mfululizo 'The Blues' hao walishindwa kupata bao licha ya kuwa na mashuti 14 yaliyolenga lango na wamefanikiwa kufunga mabao matano pekee katika mechi tano za Ligi Kuu msimu huu.

Akizungumza na tovuti rasmi ya klabu baada ya sare hiyo, Pochettino alibainisha matatizo ya Chelsea mbele ya lango kuwa ndio msingi wa kushindwa kwao kushinda michezo.

"Nafikiri tena tunatakiwa kukamilisha nafasi ambazo tunatengeneza. Katika dakika 20 au 25 za kwanza tulistahili kufunga, lakini hatukupata bao.

"Mwishowe mchezo ulikuwa wazi, katika dakika 15 au 20 za mwisho, nadhani tulitaka kushinda, wakati mwingine tulianza kuharibu safu yetu kwa sababu beki wa pembeni alikuwa juu sana, jambo ambalo liliipa Bournemouth uwezekano wa kufanya mashambulizi mengine.

"Tunahitaji kustarehe zaidi. Wakati mwingine wachezaji wa ulinzi wanataka kusaidia kwa sababu hisia ni kwamba tunatengeneza nafasi, lakini hatufungi, basi tunahitaji kuwa wajanja lakini wachezaji wengi bado wanajifunza kuhusu mchezo. Hiyo hutokea wakati tunaunda timu mpya yenye maeneo mengi tunayohitaji kuboresha.



## Hag alia bei ya wachezaji sokoni

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amelaumu timu "zinazopandisha" bei ya wachezaji kwenye soko la usajili wakati klabu hiyo ya Old Trafford inavutiwa.

Ikiwa ni pamoja na nyongeza mbalimbali, United ilitumia zaidi ya pauni milioni 180 kununua wachezaji wanne wapya, pamoja na kumsajili Jonny Evans kwa uhamisho wa bure.


Walipolaumiwa kwa matumizi makubwa katika majira ya joto, ikilinganishwa na timu ya Brighton iliyoondoka Old Trafford Jumamosi na ushindi mnono wa 3-1, Ten Hag aliipuuza.

"Nadhani timu zote zinatumia fedha nyingi," alisema.

Hiyo ni kweli kwa klabu nyingi kama Chelsea, Liverpool, Manchester City, Arsenal, Newcastle United na hata West Ham.

"Brighton pia walitumia zaidi ya pauni milioni 80, lakini kwa hakika walileta karibu faida ya pauni milioni 100 katika ada za uhamisho kutoka kwa wachezaji walionunuliwa hapo awali kwa bei nafuu ambao waliwauza kwa gharama kubwa."

"Nadhani Brighton pia walitumia fedha kama kila mtu anavyofanya. Man United inapokuja, inaongezeka bei, huo pia ni ukweli," alisema Ten Hag alisema.



361,566/-

# KOCHA SINGIDA FG ACHAMBUA KIKOSI KUIMALIZA FUTURE FC

**Na Saada Akida**

HUKU akiwa na takriban siku 12 tu kabla ya kukiongoza kikosi chake ugenini nchini Misri kwenye mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Future FC, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Mjerumani Ernst Middendorp, amesema timu yake inahitaji maboresho makubwa kuelekea mchezo huo wa kuamua hatma yao katika michuano hiyo msimu huu.

**Amesema hiyo ni kutokana na baadhi ya wachezaji hawajacheza kwenye nafasi zao walizozoeleka na walikuwa na muda mfupi kuzoea mfumo wake wa uchezaji.**

Middendorp alifanya mabadiliko ya mfumo kwenye mechi hiyo ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Future FC na Singida Fountain Gate FC kuibuka na ushindi wa bao 1-0, katika mchezo uliopigwa juzi, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, hivyo kujiweka katika nafasi nzuri ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Mabadiliko aliyoyafanya yalikuwa kuwabadilisha nafasi zao baadhi ya wachezaji ambapo Gadiel Michael ambaye ni beki wa kushoto alicheza kiungo mkabaji, Aziz Andambwile kiungo mkabaji akipanda kucheza namba nane huku France Kazadi akicheza winga ya kulia badala ya mshambuliaji wa kati.

Akizungumza na Nipashe baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo huo, kocha huyo alisema kwa muda mfupi aliokaa na timu hiyo amefanikiwa kufanya mabadiliko ya mfumo ikiwamo wachezaji kuwabadilisha nafasi zao na kucheza vizuri kama alivyotaka.

Alisema kikosi chake kinahitaji maboresho makubwa kwa kubadilisha nafasi baadhi ya wachezaji kuweza kucheza nafasi tofauti tofauti ili kuingia kwenye mfumo wake wa uchezaji.

"Kuna wachezaji wapya wamekuwa na timu kwa muda mfupi kama Marouf Tchakei ametokea Togo, wengine hawakuanza msimu vizuri kama Bruno Gomes, hawajacheza vizuri lakini wale niliowabadilishia nafasi zao wameweza kufanya vizuri," alisema kocha huyo.

Alisema kwenye mchezo huo beki Gadiel kwake ndio nyota bora wa mechi licha kubadilishiwa nafasi ya kucheza kutoka mlinzi wa kushoto hadi kiungo mkabaji, alikuwa bora na alishinda mipira mingi.

Kocha huyo aliongeza kuwa wameshamaliza dakika 90 za nyumbani katika michuano hiyo na kupata ushindi, hivyo sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye mchezo uliopo mbele yao wa Ligi Kuu Bara kabla ya kurejeana na Future FC Oktoba Mosi, mwaka huu.

"Hatuna muda wa kupoteza baada ya mechi na Future FC kumalizana na kupata ushindi sasa tunarudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi yaliyojitokeza ili kujiweka sawa kuelekea mechi yetu dhidi ya Azam FC," alisema.

Aliongeza kuwa wanahitaji kuwa makini katika ligi kwa sababu hawako sawa kutokana na kukusanya alama mbili kati ya sita, matokeo ambayo si mazuri kwa upande wao.

Singida Fountain Gate FC inatarajia kuwa ugenini kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, Alhamisi wiki hii katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

## Gamondi aionya

INATOKA UK. 24

Aliongeza kuwa amefurahishwa kuona mashabiki walivyojitokeza nchini Rwanda na anatarajia kuwaona tena kwa wingi katika mechi zote ikiwamo ya ligi dhidi ya Namungo FC ambayo ni muhimu kushinda kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kutaka kutetea ubingwa wao.

Naye mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize, alisema tayari kazi moja wameshaimaliza na sasa wanafuta matokeo hayo kwa nguvu na akili zao wanazielekeza katika mchezo wa maruadiano watakaocheza Uwanja wa Azam Complex.

Alisema wanauhitaji, hivyo wataendelea kufanya vizuri katika mchezo huo ili kufuzu na kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo baada ya miaka mingi kutofikia hatua hiyo.

"Ni kweli tumeshinda ugenini, lakini haitufanyi kuona mechi ya marudiano ni nyepesi bali tunaenda kupambana kwa ajili ya kutafuta nafasi ya kufuzu na kucheza makundi," alisema Mzize.

Yanga wanatarajia kucheza mchezo huo wa marudiano dhidi ya Al-Merrikh Septemba 30, mwaka huu, katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo, Yanga inahitaji sare yoyote ama kutoruhusu kupoteza kwa zaidi ya bao 1-0, ili kufuzu hatua ya makundi ambayo hajawahi kucheza hatua hiyo kwa miaka 24 sasa.



Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Ernst Middendorp

## Baleke aahidi mvua...

INATOKA UKURASA 24

VAR kwa sababu tumeona bao la kwanza halikuwa halali, lakini tunaamini haya yaliyotokea yatatujenga kwenye mechi inayofuata tarehe moja, tuna wiki mbili mbele, tuna mechi dhidi ya Coastal Union Alhamisi nayo itakuwa ni kama mazoezi kuelekea kwenye mchezo huo," alisema.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/23 | 17:00 | Middlesbrough FC vs Southampton FC | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02. 23/09/23 | 17:00 | Dundee FC vs Kilmarnock FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 03. 23/09/23 | 17:00 | Airdrieonians FC vs Raith Rovers FC | 2.43 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 23/09/23 | 17:15 | CA Osasuna vs Sevilla FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 05. 23/09/23 | 19:30 | Burgos CF vs Elche CF | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 06. 23/09/23 | 19:30 | Werder Bremen vs FC Cologne | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 07. 23/09/23 | 19:45 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.55 | 3.55 | 2.47 |
| 08. 23/09/23 | 20:00 | Casa Pia Lisbon vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 09. 23/09/23 | 22:00 | Stade Brest 29 vs Olympique Lyon | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 10. 24/09/23 | 14:00 | FC Metz vs Strasbourg Alsace | 2.85 | 3.20 | 2.42 |
| 11. 24/09/23 | 15:30 | Ajax Amsterdam vs Feyenoord Rotterdam | 2.48 | 3.60 | 2.50 |
| 12. 24/09/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs Union Saint-Gilloise | 2.65 | 3.40 | 2.45 |
| 13. 24/09/23 | 17:15 | Real Oviedo vs Real Valladolid | 2.75 | 2.85 | 2.70 |
| 14. 24/09/23 | 17:15 | Rayo Vallecano vs Villarreal CF | 2.55 | 3.40 | 2.55 |
| 15. 24/09/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.65 | 3.45 | 2.43 |
| 16. 24/09/23 | 21:45 | Torino FC vs AS Roma | 2.85 | 2.95 | 2.55 |
| 17. 24/09/23 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.65 | 3.35 | 2.47 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 19/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2363 | Busan I Park vs Ansan Greeners | 1.47 | 3.93 | 5.65 |
| 13:30 | 1796 | Seongnam Ilhwa vs Sangju Sangmu | 3.42 | 3.37 | 1.92 |
| 13:30 | 4048 | Cheongju FC vs Seoul E Land | 2.16 | 3.17 | 3.02 |
| 15:00 | 2100 | FC Krasnodar vs Dinamo Moscow | 2.08 | 3.62 | 2.91 |
| 15:00 | 3201 | Urartu vs Van Yerevan | 1.33 | 4.68 | 7.33 |
| 17:15 | 2223 | Nizhny Novgorod vs Spartak Moscow | 3.20 | 3.46 | 2.00 |
| 17:35 | 2550 | Rustaq Club vs Al Seeb | 3.75 | 2.80 | 2.01 |
| 18:00 | 1753 | Miedz II vs ZKS Stal Rzeszow | 8.79 | 4.91 | 1.28 |
| 18:00 | 4551 | Shirak Gyumri vs Ararat Armenia | 7.60 | 4.50 | 1.30 |
| 19:00 | 5376 | Al Ahly Cairo vs Al Masry Club | 1.43 | 4.37 | 6.36 |
| 19:30 | 1403 | Arezzo vs Olbia Calcio | 2.68 | 3.16 | 2.63 |
| 19:30 | 2048 | ASD Pineto Calcio vs Rimini | 2.72 | 3.14 | 2.61 |
| 19:30 | 3617 | US Pergolettese vs Triestina | 2.14 | 3.24 | 3.40 |
| 19:30 | 3644 | Vis Pesaro vs Virtus Entella | 3.76 | 3.29 | 2.00 |
| 19:30 | 4490 | Fermana FC vs Recanatese | 2.14 | 3.24 | 3.40 |
| 19:30 | 5673 | Lucchese vs Gubbio | 2.41 | 3.19 | 2.93 |
| 19:45 | 3149 | AC Milan vs Newcastle | 2.44 | 3.42 | 2.58 |
| 19:45 | 3571 | BSC Young Boys vs RB Leipzig | 4.75 | 4.16 | 1.56 |
| 20:30 | 1959 | Cape Town Spurs vs Golden Arrows | 3.95 | 3.23 | 1.90 |
| 20:30 | 5498 | Stellenbosch vs Moroka Swallows FC | 2.39 | 2.93 | 3.03 |
| 20:30 | 5705 | Richards Bay FC vs Chippa Utd | 2.57 | 2.93 | 2.78 |
| 21:00 | 4608 | Oxford Utd vs MK Dons | 1.70 | 3.73 | 4.08 |
| 21:45 | 1459 | Chesterfield vs Halifax | 1.60 | 3.87 | 4.96 |
| 21:45 | 1802 | Oldham vs York City | 2.04 | 3.47 | 3.26 |
| 21:45 | 1825 | Solihull Moors vs AFC Fylde | 1.98 | 3.61 | 3.30 |
| 21:45 | 1886 | Peterborough vs Cheltenham | 1.48 | 4.20 | 6.00 |
| 21:45 | 1961 | Barnsley vs Portsmouth | 2.20 | 3.35 | 3.05 |
| 21:45 | 2252 | Cardiff vs Coventry | 2.48 | 3.27 | 2.63 |
| 21:45 | 2396 | Port Vale vs Burton | 2.00 | 3.37 | 3.52 |
| 21:45 | 2509 | Preston vs Birmingham | 2.21 | 3.07 | 3.22 |
| 21:45 | 2669 | Dagenham and Redbridge vs Bromley | 2.26 | 3.19 | 3.04 |
| 21:45 | 2828 | Southampton vs Ipswich | 2.27 | 3.37 | 2.83 |
| 21:45 | 3770 | Barnet vs Aldershot | 1.58 | 3.98 | 4.96 |
| 21:45 | 3790 | Boreham Wood vs Rochdale | 2.46 | 3.20 | 2.74 |
| 21:45 | 3873 | Altrincham vs Hartlepool | 2.30 | 3.51 | 2.74 |
| 21:45 | 4363 | Woking vs Ebbsfleet | 1.88 | 3.56 | 3.67 |
| 21:45 | 4626 | Dorking Wanderers vs Wealdstone | 2.50 | 3.46 | 2.52 |
| 21:45 | 4846 | Eastleigh vs Oxford City | 2.12 | 3.46 | 3.10 |
| 21:45 | 4903 | Perugia vs Pontedera | 2.02 | 3.25 | 3.72 |
| 21:45 | 4961 | QPR vs Swansea | 2.63 | 3.28 | 2.47 |
| 21:45 | 5391 | Southend vs Maidenhead U | 1.69 | 3.61 | 4.64 |
| 21:45 | 5512 | Bristol City vs Plymouth | 1.91 | 3.51 | 3.56 |
| 21:45 | 5554 | Bristol Rovers vs West Ham U21 | 1.71 | 3.77 | 3.98 |
| 22:00 | 1728 | Paris St Germain vs Borussia Dortmund | 1.77 | 3.74 | 3.88 |
| 22:00 | 1771 | Feyenoord vs Celtic | 1.56 | 4.07 | 4.96 |
| 22:00 | 1812 | Sheffield Wed vs Middlesbrough | 3.17 | 3.27 | 2.14 |
| 22:00 | 1972 | Lazio vs Atletico Madrid | 2.82 | 3.17 | 2.38 |
| 22:00 | 2502 | Barcelona vs Royal Antwerp | 1.20 | 6.19 | 10.60 |
| 22:00 | 2990 | Manchester City vs Red Star Belgrade | 1.08 | 8.81 | 20.03 |
| 22:00 | 4280 | Shakhtar Donetsk vs Porto | 4.06 | 3.76 | 1.73 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Septemba 19, 2023
Nipashe



Arteta aanika sababu kubadili makipa UKURASA 21



Jean Baleke.

# BALEKE AAHIDI MVUA YA MABAO DYANAMOS DAR

## Uongozi nao wasema itakuwa balaa, wawaita mashabiki kushuhudia...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba, Jean Baleke, aliyekosa mabao mengi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi iliyopita dhidi ya Power Dyanamos ya Zambia, amesema atarekebisha makosa yake na kuahidi kuwa atafunga mabao mengi katika mechi ya marudiano itakayochezwa Oktoba Mosi, mwaka huu, huku akiwaomba wanachama na mashabiki kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Beleke amekiri kukosa mabao ambayo yangeweza kuifanya Simba kuibuka na ushindi, lakini akasema yote hayo yamepita na anaangalia mechi ya marudiano ambayo Simba itacheza nyumbani, akiahidi kufunga idadi kubwa ya mabao kwenye mguu wake ili kuwafurahisha na kuwapoza wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

> **"Hii imeisha, tunaangalia mechi ya nyumbani, pale nyumbani tutawafunga mabao mengi, na mimi nitafunga mabao mengi mechi ya marudiano," alisema Baleke.**

Alisema matokeo ya sare ya mabao 2-2 waliyoyapata ugenini ni mazuri na kwa sasa wana matumaini makubwa ya kwenda hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara nyingine tena msimu huu.

"Baada ya sare hii matumaini ni makubwa ya sisi kuingia makundi, nawaomba tu wanachama na mashabiki waje kwa wingi uwanjani kwa ajili ya kutupa sapoti, sisi tutawafurahisha pia," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula amekiri kuwa kuna baadhi ya maeneo kwenye kikosi itabidi yafanyiwe kazi.

"Tukubali kuwa kuna kazi ya kufanya ili kufanya vema kwenye mchezo unaokuja, sasa ndiyo tumeona uzuri wa kikosi kipana, umeona katika mechi ya Jumamosi kipindi cha kwanza na tulivyocheza cha pili timu ilibadilika sana, kuna maeneo tumefurahi, lakini tumeona kuna baadhi ya maeneo ya kufanyiwa kazi, mwalimu ameliona na nadhani atalifanyia kazi.

Na ikumbuke pia kuwa mechi ya marudiano itakuwa kipimo bora kwenda katika mechi ya African Football League dhidi ya Al Ahly Oktoba 20. Ikumbukwe kama hiki kikosi bado kina wachezaji wengi wageni ambao hawana hata miezi mitatu, bado kinaendelea kujijenga," alisema Kajula.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo pia alilalamikia bao la kwanza la Power Dynamos katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola Zambia kuwa halikuwa halali kwani mpira ulikuwa umeshatoka nje.

"Mechi ilikuwa nzuri na ngumu, Power Dynamos ni timu nzuri na ina wachezaji wenye vipaji, ilikuwa ina mchanganyiko, kipindi cha kwanza walicheza vizuri zaidi yetu sisi, kipindi cha pili tulicheza vizuri sana, lakini pia mpira ni mchezo wa makosa mara nyingine ni bahati, nadhani umeona jinsi tulivyokosa mabao mengi sana, hatutaki kulalamika, lakini ndiyo umuhimu wa kuwa na vitu kama

INAENDELEA UKURASA 23

## Gamondi aionya Yanga, ataka mabao Namungo

**Na Saada Akida**

BAADA ya kurejea nchini wakitokea Rwanda, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Angel Gamondi amewataka wachezaji wake kutobweteka na ushindi walioupata dhidi ya Al-Merrikh na badala yake sasa kuzielekeza nguvu na akili zao kwenye mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC.

Yanga itashuka katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kesho kuikaribisha Namungo FC katika mechi hiyo ya Ligi Kuu, ikitoka kuibanjua Al-Merrikh ugenini mabao 2-0 kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Akizungumza baada ya timu hiyo kutua nchini ikitokea Rwanda ilipochezwa mechi yao dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan, Gamondi alisema amewataka wachezaji wake kujiona ni bora kuliko timu nyingine baada ya kufanikiwa kupata ushindi dhidi ya Wasudan hao, lakini hawapaswi kujisahau kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu.

Alisema katika mchezo huo walicheza vizuri na kutengeneza nafasi nyingi kwa kupata ushindi wa mabao 2-0 mbele ya timu nzuri na sasa wachezaji wanatakiwa kusahau matokeo hayo na kujipanga kwa mechi ijayo ya Ligi Kuu.

"Tunafuraha kwa matokeo tuliyopata Rwanda, wachezaji walicheza vizuri tumepata nafasi nyingine, lakini sasa tunaangalia mechi iliyopo mbele yetu kuhakikisha tunaendelea pale tulipoishia kwa kutafuta ushindi wa idadi kubwa ya mabao.

"Nimeongea na wachezaji kuhakikisha wanasahau matokeo ya mechi zilizopita na kuingia uwanjani kucheza kwa tahadhari kubwa, kupata matokeo mazuri dhidi ya Namungo FC," alisema kocha huyo.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >